JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI (PSLE ) 2020

## KISWAHILI

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI (PSLE) 2020

# KISWAHILI

Kimechapishwa na:
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2021

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO


DIBAJI ........................................................................................................ iv

1.0 UTANGULIZI .................................................................................... 1

2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA .................................... 1

2.1 Sehemu A: Sarufi .............................................................................. 2

2.2 Sehemu B: Lugha ya Kifasihi ........................................................... 30

2.3 Sehemu C: Ushairi ............................................................................ 44

2.4 Sehemu D: Utungaji .......................................................................... 54

2.5 Sehemu E: Ufahamu ......................................................................... 58

3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA UFAULU KWA WATAHINIWA KATIKA MADA MBALIMBALI .................................................................... 69

4.0 HITIMISHO ......................................................................................... 70

5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO ............................................................ 71

KIAMBATISHO A ...................................................................................... 73

KIAMBATISHO B ...................................................................................... 75

## DIBAJI

Taarifa ya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kwa somo la Kiswahili mwaka 2020, imeandaliwa na Baraza la Mitihani la Tanzania. Lengo la taarifa hii ni kutoa mrejesho kwa watunga sera, wathibiti ubora wa shule, walimu, wanafunzi, watunga mitaala na wadau wengine wa elimu,kuhusu umahiri walionao wanafunzi katika kujibu maswali na changamoto zilizowakabili.

Taarifa hii imeainisha mambo mbalimbali yaliyochangia watahiniwa kujibu maswali kwa usahihi ikiwa ni pamoja na kuelewa matakwa ya swali pamoja na kuwa na maarifa ya kutosha katika mada mbalimbali za somo la Kiswahili, jambo linaloonesha kuwa ufundishaji na ujifunzaji ulifanyika vizuri. Aidha sababu za watahiniwa kushindwa kujibu maswali kwa usahihi, ni pamoja na kushindwa kutambua matakwa ya swali, kukosa maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya msamiati na aina za maneno. Sababu nyingine ni kuchagua jibu zaidi ya moja katika kujibu maswali mbalimbali kinyume na maelekezo. Pia, watahiniwa walishindwa kupanga sentensi katika mtiririko unaoleta mantiki ili kuunda kifungu cha maneno. Mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila swali umeainishwa katika uchambuzi huu kwa kutumia maelezo, jedwali na vielelezo.

Baraza la Mitihani la Tanzania lina imani kuwa, mrejesho huu utawawezesha wadau mbalimbali wa elimu kutafuta mbinu stahiki na kuchukua hatua madhubuti ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji.

Mwisho, Baraza la Mitihani la Tanzania linatoa shukrani za dhati kwa wote walioshiriki ipasavyo katika kuandaa taarifa hii.

Dkt. Charles E. Msonde<br>
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Mtihani wa Kiswahili wa kumaliza Elimu ya Msingi 2020 ulikuwa na maswali **arobaini na tano** (**45**). Maswali **arobaini** (**40**) yalikuwa ya kuchagua jibu sahihi na kila swali lilikuwa na alama **moja** (**01**). Maswali hayo yaligawanyika katika sehemu **nne** (**04**), kama ifuatavyo: Sehemu A *Sarufi*; B *Lugha ya Kifasihi*; C *Ushairi* na D *Utungaji*. Aidha, kulikuwa na maswali **matano (05)** ya kujieleza kutoka sehemu E *Ufahamu* ambayo yalikuwa na alama **mbili (02)** kwa kila swali.

Jumla ya watahiniwa **1,023,950** walisajiliwa kufanya mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi (**PSLE**) **2020** kwa somo la Kiswahili. Waliofanya mtihani walikuwa **1,009,519.** Watahiniwa waliofaulu mtihani huu ni **884**,**034**, sawa na asilimia **87.68**.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa umefanyika kwa kuainisha maswali yote ya mtihani, yaani maswali ya kuchagua herufi ya jibu sahihi na yale ya majibu mafupi. Uchambuzi huu unaonesha majibu yaliyotolewa na watahiniwa kwa kila swali kwa kuzingatia idadi na asilimia ya watahiniwa waliochagua kila chaguo. Uchambuzi wa takwimu umewasilishwa kwa njia ya jedwali na vielelezo. Rangi mbalimbali zimetumika kuonesha viwango vya ufaulu na asilimia ya watahiniwa kwa kila swali. Rangi nyekundu imetumika kuwakilisha kiwango hafifu cha ufaulu yaani **0 – 39**. Rangi ya njano imetumika kuwakilisha kiwango cha wastani cha ufaulu, yaani asilimia **40 – 59** na rangi ya kijani imetumika kuwakilisha kiwango kizuri cha ufaulu, yaani asilimia **60 – 100**. Aidha, alama ***** imetumika katika jedwali na vielelezo kuonesha jibu sahihi kwa kila swali. Vilevile, watahiniwa waliochagua jibu zaidi ya moja au hawakuchagua chaguo lolote wameoneshwa kwa neno “mengine”.

## 2.1 Sehemu A: Sarufi

Sehemu hii ilikuwa na maswali ishirini (20) yaliyomtaka mtahiniwa kuonesha uwezo wa kutambua kauli mbalimbali za vitenzi, maana ya msamiati, matumizi ya nafsi, nyakati mbalimbali, hali na aina za maneno.

**Swali la 1:** "Amevaa kichina, mimi nimevaa kihindi." "kichina na kihindi" ni aina gani za neno?

A Vielezi

B Vivumishi

C Viwakilishi

D Vihusishi

E Nomino.

Swali lilitoka katika mada ya Sarufi na lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kutambua aina za maneno kama yalivyotumika katika sentensi. Jedwali Na. 1 linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

**Jedwali Na. 1: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo**

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 44,2314 | 186,649 | 115,743 | 25,257 | 234,444 | 6,791 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 43.74 | 18.46 | 11.45 | 2.50 | 23.18 | 0.67 |

Kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa cha wastani, ambapo watahiniwa 442,314 sawa na asilimia 43.74 walichagua jibu sahihi A Vielezi. Hii inadhihirisha kwamba watahiniwa hao walikuwa na uelewa juu ya "vielezi" kuwa huelezea zaidi kuhusu tendo lilivyotendeka. Hivyo, watahiniwa hao waliweza kubaini maneno "kichina na kihindi" kuwa ni vielezi vinavyoelezea zaidi kitenzi "amevaa".

Hata hivyo, watahiniwa 562,093 sawa na asilimia 55.60 hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu “vielezi” hivyo walichagua vipotoshi ambavyo ni B *Vivumishi*, C *Viwakilishi,* D *Vihusishi* na E *Nomino.* Watahiniwa waliochagua *Vivumishi,* walishindwa kutambua kuwa neno hilo halitoi taarifa juu ya tendo lilivyotendeka bali linatoa taarifa zaidi kuhusu nomino au kiwakilishi katika sentensi. Pia, uteuzi wa *Viwakilishi* unatokana na watahiniwa kuhusisha maneno “kichina na kihindi” kuwa huwakilisha majina ya kichina na kihindi hivyo kudhani kuwa ni *viwakilishi* kama aina za maneno. Vilevile, uteuzi wa *vihusishi* ni ushahidi kuwa watahiniwa hawakuwa na maarifa kuwa vihusishi huhusisha maneno mawili au zaidi katika sentensi. Aidha, uteuzi wa *nomino* umetokana na watahiniwa kutokufahamu kwamba *nomino* ni neno linalotaja majina ya watu, vitu au mahali. Walidhani kuwa neno “Kichina” na “Kihindi” yapo kuwakilisha Lugha lakini kwa muundo wa sentensi maneno hayo hayakutumika kuwakilisha Lugha. Kwa ujumla, uteuzi wa vipotoshi hivyo unadhihirisha kuwa, watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu aina za maneno.

**Swali la 2:** “Wewe ni mtoto mzuri sana.” Neno lililotumika kama kiwakilishi ni lipi?

A mtoto

B ni

C mzuri

D sana

E wewe.

Swali hili lilitoka katika mada ya Sarufi na lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kutambua aina za maneno kama yalivyotumika katika sentensi. Jedwali Na. 2 linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

**Jedwali Na. 2: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo**

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 76,657 | 96,746 | 149,877 | 42,676 | 638,749 | 6,493 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 7.58 | 9.57 | 14.82 | 4.22 | 63.17 | 0.64 |

Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri kwa kuwa watahiniwa 638,749 sawa na asilimia 63.17 walichagua jibu sahihi E *wewe*. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu aina za maneno hivyo waliweza kubaini kuwa neno "*wewe"* ni kiwakilishi cha nafsi ya pili umoja ambacho huwakilisha nomino ambayo hutaja majina ya watu, vitu au mahali.

Watahiniwa 365,956 sawa na asilimia 36.20 walichagua vipotoshi ambavyo ni A *mtoto,* B *ni,* C *mzuri,* na D *sana.* Watahiniwa waliochagua *mtoto,* walishindwa kuelewa kuwa neno *mtoto* ni nomino inayopatikana katika upande wa kiarifu katika sentensi. Aidha, uteuzi wa neno *ni* unatokana na watahiniwa kushindwa kuelewa kuwa neno hilo ni kitenzi kishirikishi ambacho hutoa taarifa iliyokamili katika sentensi. Vilevile, uteuzi wa neno *mzuri* unaonesha kuwa watahiniwa walishindwa kuelewa kuwa neno hilo ni kivumishi kinachotoa taarifa zaidi kuhusu nomino au kiwakilishi. Pia, uteuzi wa neno *sana*, unaonesha kuwa watahiniwa walishindwa kuelewa kuwa neno "sana" ni kielezi ambacho kinatoa taarifa kuhusu jinsi tendo lilivyotendeka. Uteuzi wa vipotoshi hivyo unathibitisha kuwa, watahiniwa hao hawana uelewa kuhusu maana ya nomino, kitenzi, kivumishi na kielezi na hawaelewi matumizi sahihi ya maneno hayo katika sentensi.

**Swali la 3:** "Walimu wanafundisha lakini wanafunzi hawajisomei" neno "lakini" ni aina gani ya neno?

A Kivumishi

B Kiunganishi

C Kitenzi

D Kielezi

E Kihisishi.

Swali hili lilitoka katika mada ya Sarufi na lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kutambua aina za maneno na matumizi yake katika sentensi. Jedwali Na. 3 linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

**Jedwali Na. 3: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo**

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 66,144 | 671,303 | 89,793 | 134,434 | 42,558 | 6,966 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 6.54 | 66.39 | 8.88 | 13.29 | 4.21 | 0.69 |

Kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri kwa kuwa watahiniwa 671,307 sawa na asilimia 66.39 walichagua jibu sahihi B *Kiunganishi.* Watahiniwa hao, walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu aina za maneno hivyo kuweza kubaini kuwa neno "lakini" ni kiunganishi ambacho huunganisha sentensi mbili au zaidi.

Hata hivyo, watahiniwa 332,929 sawa na asilimia 32.9 walichagua vipotoshi: A *Kivumishi*, C *Kitenzi*, D *Kielezi* na E *Kihisishi*. Watahiniwa waliochagua *Kivumishi* walishindwa kuelewa kuwa *kivumishi* hutoa taarifa zaidi kuhusu nomino au kiwakilishi katika sentensi. Aidha, waliochagua *Kitenzi* walishindwa kuelewa kuwa *Kitenzi* ni neno linaloelezea matendo au kutendeka kwa jambo.

Waliochagua *Kielezi,* walishindwa kubaini kuwa neno hilo hutumika kuelezea jinsi tendo lilivyotendeka. Vilevile, waliochagua *Kihisishi* walishindwa kubaini kuwa ni neno linaloonesha vionjo vya moyo na kugusa hisia za watu. Kwa jumla, uteuzi wa vipotoshi hivyo umetokana na watahiniwa kukosa uelewa kuhusu aina za maneno, hususani kiunganishi.

**Swali la 4** "Amenunua bidhaa kadhaa na kuzipeleka nyumbani."
Neno "kadhaa" ni aina gani ya neno?

A Kielezi
B Kitenzi
C Nomino
D Kiwakilishi
E Kivumishi.

Swali hili lilitoka katika mada ya Sarufi na lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kutambua aina za maneno kama yalivyotumika katika sentensi. Jedwali Na. 4 linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.

**Jedwali Na. 4: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo**

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 277,072 | 130,932 | 136,013 | 168,852 | 289,259 | 9,070 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 27.40 | 12.95 | 13.45 | 16.70 | 28.61 | 0.90 |

Kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa hafifu kwani watahiniwa 712,869 sawa na asilimia 70.5 walichagua vipotoshi A *Kielezi*, B *Kitenzi*, C *Nomino* na D *Kiwakilishi*. Watahiniwa waliochagua *Kielezi* walishindwa kubaini kuwa, neno hilo hutumika kuelezea zaidi kitenzi, kivumishi au kielezi kingine. Aidha, Uteuzi wa *kitenzi* ulitokana na kushindwa kubaini kuwa neno hilo huarifu juu ya ufanyikaji wa tendo, waliochagua *nomino*

walihusisha neno hilo na “nomino” ambayo hutaja majina ya watu, vitu au mahali. Pia, uteuzi wa *kiwakilishi*, ulitokana na watahiniwa kuhusisha neno *kadhaa* na nomino bila kuangalia mazingira ya utokeaji wa neno hilo katika muundo wa sentensi. Hivyo, uteuzi wa vipotoshi hivyo umetokana na watahiniwa kukosa maarifa mahususi kuhusu vivumishi.

Uchambuzi naonesha kuwa, watahiniwa 289,259 sawa na asilimia 28.61 walichagua jibu sahihi E *Kivumishi*. Hii inathibitisha kuwa, watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu vivumishi kuwa ni maneno yanayoelezea nomino au kiwakilishi katika sentensi ambapo kivumishi “kadhaa” kimeelezea zaidi kuhusu nomino “bidhaa”.

**Swali la 5:** “Madaktari walifanya kila njia ili kunusuru maisha yake.” Neno “ili” ni aina gani ya neno?

A Kihisishi

B Kihusishi

C Kiunganishi

D Kielezi

E Kiwakilishi.

Swali hili lilitoka katika mada ya Sarufi na lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kutambua aina za maneno kama yalivyotumika katika sentensi. Jedwali Na. 5 linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo

**Jedwali Na. 5: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo**

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 85,481 | 92,298 | 602,238 | 135,263 | 87,268 | 8,650 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 8.52 | 9.13 | 59.62 | 13.41 | 8.63 | 0.90 |

Kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa cha wastani, kwani watahiniwa 602,238 sawa na asilimia 59.62 walichagua jibu sahihi C *Kiunganishi*. Hii inathibitisha kuwa, watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu "kiunganishi" ambapo waliweza kufahamu kuwa ni neno au maneno yanayounganisha neno moja na jingine au sentensi zaidi ya moja.

Watahiniwa 400,310 sawa na asilimia 39.5 walichagua vipotoshi, A *Kihisishi,* B *Kihusishi,* D *Kielezi* na E *Kiwakilishi.* Waliochagua Kihisishi walishindwa kubaini kuwa ni neno linaloonesha vionjo vya moyo na kugusa hisia za watu. Aidha, uteuzi wa *kihusishi* unaonesha kuwa watahiniwa hawakuelewa kuwa kihusishi uhusisha maneno mawili au zaidi yenye hadhi tofauti. Vilevile, waliochagua *Kielezi* walishindwa kubaini kuwa, neno hilo hutumika kuelezea zaidi jinsi tendo lilivyotendeka. Pia, waliochagua *kiwakilishi* walishindwa kuelewa kuwa ni aina ya maneno ambayo huwakilisha nomino katika sentensi. Uchaguzi wa vipotoshi hivyo unaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na maarifa kuhusu kiunganishi na matumizi yake katika sentensi.

**Swali la 6:** "Watoto wawili waliimba wimbo vizuri sana." Neno "wawili" ni aina gani ya neno?

A Kiunganishi

B Kiwakilishi

C Kivumishi

D Kielezi

E Kitenzi.

Swali hili lilitoka katika mada ya Sarufi na lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kutambua aina za maneno kama yalivyotumika katika sentensi. Jedwali Na. 6 linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.

**Jedwali Na. 6: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo**

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 79,791 | 248,881 | 416,921 | 185,087 | 72,742 | 7,776 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 7.89 | 24.61 | 41.23 | 18.30 | 7.19 | 0.77 |

Kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa cha wastani. Watahiniwa 416,921 sawa na asilimia 41.23 walichagua jibu sahihi ambalo ni C *Kivumishi.* Hii inadhihirisha kuwa watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu “kivumishi” ambapo walielewa kuwa kivumishi ni neno au maneno ambayo huelezea zaidi kuhusu nomino au kiwakilishi katika sentensi.

Hata hivyo, watahiniwa 586,501 sawa na asilimia 58.00 walichagua vipotoshi A *Kiunganishi,* B *Kiwakilishi,* D *Kielezi* na E *Kitenzi.* Waliochagua *Kiunganishi* walishindwa kubaini kuwa kiunganishi ni neno au maneno ambayo huunganisha neno na neno au kikundi kimoja cha maneno na kingine. Uteuzi wa kipotoshi *Kiwakilishi* unaonesha kuwa watahiniwa walishindwa kuelewa kuwa *kiwakilishi* ni aina ya maneno ambayo huwakilisha nomino katika sentensi. Aidha, waliochagua *Kielezi* walishindwa kubaini kuwa, neno hilo hutumika kuelezea zaidi kitenzi, kivumishi au kielezi kingine. Pia, waliochagua *Kitenzi* walishindwa kuelewa kuwa *kitenzi* ni neno linalotaja tukio au tendo linavyotendeka. Uchaguzi wa vipotoshi hivyo unathibitisha kuwa watahiniwa wa kundi hili hawakuwa na maarifa ya kubaini kivumishi kama kilivyotumika katika sentensi waliyopewa.

**Swali la 7:** Neno lipi **halihusiani** na maneno mengine kati ya haya yafuatayo?

A Wali

B Ugali

C Ndizi

D Viazi

E Mchicha.

Swali hili lilitoka katika mada ya Sarufi na lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kufahamu maana ya msamiati katika lugha ya Kiswahili. Jedwali Na. 7 linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.

**Jedwali Na. 7: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo**

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 33,595 | 41,313 | 200,303 | 39,554 | 687,611 | 8,822 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 3.32 | 4.09 | 19.81 | 3.91 | 68.00 | 0.87 |

Watahiniwa walikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu katika swali hili kwani watahiniwa 687,611 sawa na asilimia 68.00 walichagua jibu sahihi E *Mchicha.* Watahiniwa hao walielewa kuwa *Wali*, *Ugali*, *Ndizi* na *Viazi* ni vyakula jamii ya wanga lakini *Mchicha* ni mboga jamii ya vitamini. Hivyo, walikuwa na uelewa juu ya msamiati wa Lugha ya Kiswahili.

Aidha, watahiniwa 314,765 sawa na asilimia 31.1 walichagua vipotoshi A *Wali*, B *Ugali*, C *Ndizi* na D, *Viazi.* Watahiniwa hao walishindwa kuelewa kuwa wali, ugali,ndizi na viazi ni vyakula jamii ya wanga na hufanya kazi ya kuupa nishati mwili wa binadamu lakini mchicha ni jamii ya vitamini. Hivyo, watahiniwa hao walishindwa kubaini kuwa mchicha ndio neno lililotofauti na maneno mengine.

**Swali la 8:** Kuku, bata, mwewe, kunguru na kanga kwa neno moja wanaitwaje?

A Wanyama


B Ndege

C Wadudu

D Wanyamapori

E Ndegepori.

Swali hili lilitoka katika mada ya Sarufi na lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kuhusu matumizi ya msamiati katika lugha ya Kiswahili. Kielelezo Na. 1 kinaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.




*Kielelezo Na. 1: Asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo*

Kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri ambapo watahiniwa 873,500 sawa na asilimia 86.38 walichagua jibu sahihi B *Ndege.* Watahiniwa hao waliweza kubaini kuwa *kuku, bata, mwewe, kunguru* na *kanga* ni viumbe wenye manyoya na mabawa na midomo iliyochongoka, hutaga mayai na huweza kuruka angani, ambao kwa jina moja huitwa ndege. Hivyo, watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha juu ya maana ya msamiati ndege.

Watahiniwa wengine 131,555 sawa na asilimia 13.0 walishindwa kubaini neno moja linalojumuisha kuku, bata, mwewe, kunguru na kanga hivyo kuandika kipotoshi *wanyama* ambao huwa na sifa ya kutokuwa binadamu, mdudu wala mmea na ambao wana miguu minne. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *wadudu* walishindwa kuelewa kuwa *wadudu* ni viumbe wadogo waliogawanyika katika sehemu tatu ambazo ni kichwa, kiwiliwili na tumbo, pia wana miguu sita na hawana uti wa mgongo. Aidha, waliochagua wanyamapori hawakuwa na uelewa kuwa wana *sifa ya kutokuwa binadamu, mdudu wala mmea, wana miguu minne na hupendelea kuishi porini*. Vilevile, waliochagua ndegepori hawakuelewa kuwa ni kiumbe mwenye manyoya na mabawa, mdomo uliochongoka, hutaga mayai ,na huweza kuruka angani na hupendelea kuishi porini. Hivyo, watahiniwa hao walikosa maarifa kuhusu maana na matumizi ya msamiati "ndege" kama linavyotumika katika Lugha ya Kiswahili.

**Swali la 9:** Neno lipi halilandani na mengine kati ya yafuatayo?

A Mchungwa
B Embe
C Ndizi
D Papai
E Pera.

Swali hili lilitoka katika mada ya Sarufi na lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kuhusu maana ya msamiati katika lugha ya Kiswahili. Jedwali Na. 8 linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.

**Jedwali Na. 8: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo**

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 608,442 | 26,877 | 251,334 | 28,409 | 87,528 | 8,608 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 60.17 | 2.66 | 24.86 | 2.81 | 8.66 | 0.85 |

Kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri kwani watahiniwa 608,442 sawa na asilimia 60.17 walichagua jibu sahihi A *Mchungwa.* Watahiniwa hao walielewa kuwa *embe*, *ndizi*, *papai* na *pera* yote ni matunda isipokuwa mchungwa ambao ni mti unaozaa matunda ya machungwa. Hivyo, watahiniwa waliweza kuelewa maana ya msamiati na kuweza kuchagua jibu sahihi.


Hata hivyo watahiniwa 394,148 sawa na asilimia 39.00 walichagua vipotoshi B *Embe,* C *Ndizi,* D *Papai na* E *Pera*. Uteuzi wa vipotoshi hivyo ulitokana na watahiniwa kushindwa kuelewa kuwa *embe*, *ndizi*, *papai* na *pera* ni matunda japokuwa yana ladha tofauti lakini mchungwa ni mti unaozaa matunda aina ya machungwa. Watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maana ya msamiati mchungwa, hivyo kushindwa kubaini kuwa neno hilo halilandani na mengine.

**Swali la 10:** Mtu hodari asiyeogopa huitwaje?

A Jambazi
B Jangili
C Jasiri
D Jeuri
E Njemba.

Swali hili lilitoka katika mada ya Sarufi na lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kuhusu matumizi ya msamiati “jasiri” katika lugha ya

Kiswahili. Muhtasari wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo umeoneshwa katika Kielelezo Na. 2.




*Kielelezo Na. 2: Asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo*

Kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri kwani watahiniwa 875,841 sawa na asilimia 86.62 walichagua jibu sahihi C *Jasiri* linalomaanisha mtu anayekabili mambo magumu pasipo uoga wala hofu. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maana ya msamiati “jasiri” na jinsi linavyotumiwa katika lugha ya Kiswahili.

Uchambuzi unaonesha kuwa, watahiniwa 129,067 sawa na asilimia 12.60 walichagua vipotoshi: A *Jambazi*, B *Jangili*, D *Jeuri* na E *Njemba.* Waliochagua kipotoshi *jambazi* walishindwa kuelewa kuwa, neno jambazi humaanisha mtu anayechukua mali za watu kwa nguvu kwa kutumia silaha. Vilevile, waliochagua kipotoshi *jangili* walishindwa kuelewa kuwa, *jangili* ni mtu anayewinda na kuua wanyama wa porini kwenye hifadhi za wanyama za taifa bila ya kibali kutoka serikalini. Aidha, waliochagua kipotoshi *jeuri* hawakuwa sahihi kwa kuwa, neno hilo humaanisha mtu mwenye

tabia ya uchokozi au usumbufu, kiburi, ufedhuli, au kutokuwa na utii, mwenye majivuno au kujiona bora. Pia, uteuzi wa kipotoshi *njemba* haukuwa sahihi kwani humaanisha mwanamume mwenye umbo kubwa na anayetisha au kuogopesha. Kwa ujumla, uteuzi wa vipotoshi hivyo unaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuelewa kuwa "jasiri" ni mtu anayekabiliana na mambo magumu pasipo uoga wala hofu.

**Swali la 11:** Mahali panapochimbwa madini ya chumvi, makaa ya mawe, dhahabu na almasi panaitwaje?

A Mgodi


B Handaki

C Mtoni

D Bondeni

E Shimoni.

Swali hili lilitoka katika mada ya *Sarufi* na lililenga kupima ujuzi wa watahiniwa kuhusu matumizi ya msamiati katika lugha ya Kiswahili. Kielelezo Na. 3 kinaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.




*Kielelezo Na. 3: Asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo*

Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri kwa kuwa watahiniwa 896,805 sawa na asilimia 88.69 waliweza kuchagua jibu sahihi A *Mgodi.* Watahiniwa hao walikuwa na maarifa yakutosha kuhusu maana ya msamiati "mgodi" kuwa ni eneo la ardhi panapofanyika shughuli za machimbo kama vile dhahabu, almasi chumvi na madini mengine.

Hata hivyo, watahiniwa 107,636 sawa na asilimia 10.6 walichagua vipotoshi B *Handaki,* C *Mtoni,* D *Bondeni* na E *Shimoni*. Kipotoshi *handaki* hakikuwa sahihi kwani neno handaki humaanisha shimo refu na kubwa linalochimbwa kwa lengo la kulinda, kujihami na kushambulia adui wakati wa mapambano ya silaha vitani. Vilevile, uteuzi wa kipotoshi *mtoni* haukuwa sahihi kwani humaanisha eneo ambalo kuna mtiririko mkubwa wa maji wa asili kuelekea baharini, ziwani au kwenye mto mwingine.

Aidha, uteuzi wa kipotoshi *bondeni* halikuwa sahihi kwani neno hili lina maana ya eneo la ardhi lililopo katikati ya vilima au milima miwili na huwa na mto au kijito kinachotiririsha maji ndani yake. Kipotoshi *shimoni* pia halikuwa jibu sahihi kwa sababu neno shimoni lina maana ya eneo lenye uwazi mkubwa uliopo katika ardhi, mwili au mti unaotokana na ama kuchimbwa au kuchimbika wenyewe. Kwa ujumla, uteuzi wa vipotoshi hivyo unaonesha kuwa watahiniwa hao walishindwa kuelewa kuwa mgodi ndio mahali panapochimbwa madini ya chumvi, makaa ya mawe, dhahabu na almasi.

**Swali la 12:** Neno lipi kati ya yafuatayo ni kinyume cha neno “kinai”?

A Tosheka

B Ridhika

C Shibe

D Ridhia

E Tamani.

Swali hili lilitoka katika mada ya *Sarufi* na lililenga kupima ujuzi wa watahiniwa kuhusu matumizi ya msamiati katika lugha ya Kiswahili. Jedwali Na. 9 linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

**Jedwali Na. 9: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo**.

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 218,815 | 146,655 | 96,822 | 67,656 | 471,827 | 9,423 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 21.64 | 14.50 | 9.57 | 6.69 | 46.66 | 0.93 |

Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani kwani watahiniwa 471,827 sawa na asilimia 46.66 waliweza kuchagua jibu sahihi E *Tamani.* Watahiniwa hao walikuwa na maarifa yakutosha kuhusu maana ya msamiati mbalimbali hususani kinyume cha maneno. Kwa mfano, watahiniwa hao waliweza kubaini kuwa neno “kinai” lina maana ya kosa hamu ya kutaka kitu zaidi ya ulichonacho au ridhika, hivyo kuweza kufahamu kuwa kinyume chake ni *tamani* likiwa na maana ya kupata hamu ya kufanya kitu au jambo fulani.

Aidha, uchambuzi unaonesha kuwa, watahiniwa 529,948 sawa na asilimia 52.4 walichagua vipotoshi A *Tosheka* B *Ridhika,* C *Shibe* na D *Ridhia.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi *tosheka,* hawakuelewa kuwa neno hilo lina maana sawa na neno *ridhika*

hivyo haliwezi kuwa kinyume cha neno "kinai". Vilevile, neno *ridhika,* linafafana kimaana na neno "kinai" hivyo neno hilo sio kinyume cha neno "kinai". Pia, waliochagua neno *shibe*, hawakuelewa maana ya neno hilo kuwa: ni hali ya mtu kula chakula au kunywa kinywaji cha kutosha kiasi cha kujaza tumbo lake hivyo kushindwa kuchagua jibu sahihi. Waliochagua neno *ridhia* walishindwa kuelewa kuwa neno hilo lina maana: *ruhusu jambo au kitu kifanyike au kubali utekelezaji wa jambo* hivyo neno hilo haliwezi kuwa kinyume cha neno "kinai". Kwa ujumla, watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maana na kinyume cha msamiati "kinai" kama unavyotumika katika Lugha ya Kiswahili.

**Swali la 13:** Neno lipi linakosekana katika sentensi ifuatayo? "Humo__________ alimopita mbunge wakati wa kuomba kura".

A ndipo


B ndio

C ndiko

D ndie

E ndimo

Swali hili lilitoka katika mada ya Sarufi na lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa juu ya dhana ya upatanisho wa kisarufi katika lugha ya Kiswahili. Kielelezo Na. 4 kinaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.




*Kielelezo Na. 4: Asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo*

Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri kwani asilimia 74.20 ya watahiniwa walichagua jibu sahihi E *ndimo* ambacho ni kitenzi kishirikishi kinachokamilisha sentensi yenye upatanisho wa kisarufi na kilichozingatia ngeli za nomino.

Watahiniwa 252,761 sawa na asilimia 25.0 walichagua kipotoshi A *ndipo,* B *ndio,* C *ndiko na* D *ndie.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi *ndipo*, hawakuwa na uelewa kuwa neno hilo hutumika sehemu ya wazi inayorejelea mahali fulani. Hivyo, kwa mpangilio wa maneno katika sentensi kwenye swali hilo haiwezekani neno hilo litumike kukamilisha sentensi kwa kuzingatia muktadha wa sentensi husika. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *ndio*, walishindwa kuelewa neno "ndio" hutumika kuleta upatanisho wa kisarufi wa O -rejeshi hasa katika wingi wa ngeli ya kwanza YU-A-WA. Hivyo kutokana na muundo wa sentensi katika swali, neno hilo haliwezi kuwa jibu sahihi. Uteuzi wa kipotoshi *ndiko* haukuwa sahihi kwani neno hilo ni kitenzi kishirikishi cha O –rejeshi kinachorejelea

mahali mahususi sehemu fulani, hivyo neno hilo haliwezi kuwa jibu sahihi. Aidha, waliochagua kipotoshi *ndie* walishindwa kuelewa kuwa neno hilo linarejelea mtu na sio mahali fulani hivyo haliwezi kutumika kukamilisha sentensi husika. Kwa ujumla, watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kubaini neno lenye upatanisho wa kisarufi linalokamilisha sentensi husika kwa usahihi.

**Swali la 14:** Abdi____________ mtoto wa jirani yangu. Neno linalokamilisha sentensi hii ni lipi?

A siye
B siyo
C sie
D si
E sio

Swali hili lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kutambua matumizi ya sarufi katika sentensi. Jedwali Na 10 linaonesha majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.

**Jedwali Na 10: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo**

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 122,858 | 361,429 | 33,993 | 289,859 | 195,410 | 7,649 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 12.15 | 35.74 | 3.36 | 28.66 | 19.32 | 0.76 |

Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa hafifu kwani watahiniwa 713,690 sawa na asilimia 70.5 walichagua vipotoshi
A *Siye,* B *Siyo,* C *Sie* na E *Sio.* Watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo walishindwa kuelewa kuwa si kila neno huweza kukamilisha nafasi iliyoachwa wazi, bali ni kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi. Kwa ujumla watahiniwa walioteua vipotoshi hivyo

hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya dhana ya upatanisho wa kisarufi katika lugha ya Kiswahili.

Aidha, watahiniwa 289,859 sawa na asilimia 28.66 walichagua jibu sahihi D *si*. Watahiniwa hao waliweza kuchagua jibu hilo kwa kuwa walizingatia upatanisho wa kisarufi uliopo kati ya nomino iliyopo katika upande wa kiima na kitenzi kishirikishi *si* kilichopo katika upande wa kiarifu ambacho ndicho kinachokamilisha sentensi husika. Hivyo, watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu upatanisho wa kisarufi katika sentensi za Lugha ya Kiswahili.

**Swali la 15:** Hawa________walioalikwa katika sherehe hii. Neno lipi linakamilisha sentensi hii kwa usahihi?

A ndio

B ndiyo

C ndiye

D ndiwo

E ndilo

Swali hili lilitoka katika mada ya Sarufi na lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika upatanisho wa kisarufi kwenye lugha ya Kiswahili. Jedwali Na. 11 linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

**Jedwali Na. 11: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo**

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 556,728 | 256,693 | 65,318 | 107,423 | 19,092 | 5,944 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 55.06 | 25.39 | 6.46 | 10.62 | 1.89 | 0.59 |

Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani kwa sababu asilimia 55.01 ya watahiniwa walichagua jibu sahihi A *ndio*

yaani kitenzi kishirikishi ambacho hutumika kuleta upatanisho wa kisarufi katika sentensi ambayo Kiima chake kinaundwa na kiwakilishi cha wingi kinachoonesha ukaribu. Hivyo, watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya upatanisho wa kisarufi.

Watahiniwa 448,526 sawa na asilimia 44.40 walichagua kipotoshi B *ndiyo,* C *ndiye,* D *ndiwo* na E *ndilo.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi *ndiyo*, hawakuwa na uelewa kuwa neno hilo ni kitenzi kishirikishi ambacho hutumika kuleta upatanisho wa kisarufi katika sentensi yenye Kiima kinachoundwa na kiwakilishi cha umoja kinachoonesha ukaribu. Hivyo, kwa kuzingatia muktadha wa sentensi husika neno hilo haliwezi kuwa jibu sahihi. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *ndiye*, hawakuelewa kuwa neno hilo ni kitenzi kishirikishi ambacho hutumika kuleta upatanisho wa kisarufi katika sentensi yenye Kiima kinachoundwa na kiwakilishi cha umoja kinachoonesha umbali. Hivyo, kutokana na muundo wa sentensi katika swali, hakiwezi kukamilisha sentensi hiyo kwa sahihi.

Aidha, uteuzi wa kipotoshi *ndiwo*, hauwezi kuwa sahihi kwa kuwa neno hilo halina uhusiano na maneno mengine katika sentensi husika. Pia, waliochagua kipotoshi *ndilo* walishindwa kuelewa kuwa neno hilo halina upatanisho wa kisarufi katika sentensi husika kwa sababu ni kitenzi kishirikishi kinachotumika kurejelea majina yasiyokuwa na uhai. Kwa ujumla, watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kubaini neno lenye upatanisho wa kisarufi linalokamilisha sentensi husika kwa usahihi.

**Swali la 16:** “Baba atamkanya mjomba ili aache ulevi.” Sentensi hii ipo katika wakati gani?

A Timilifu


B Ujao

C Uliopo

D Mazoea

E Uliopita.

Swali hili lilitoka katika mada ya Sarufi na lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kutambua nyakati mbalimbali katika sentensi. Kielelezo Na. 5 kinaonesha machaguo ya watahiniwa katika swali hili.




*Kielelezo Na. 5: Asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo*

Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri kwani asilimia 80.43 ya watahiniwa walichagua jibu sahihi B *Ujao.* Hii inadhihirisha kuwa, watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu nyakati mbalimbali katika sentensi za Lugha ya Kiswahili. Mathalan waliweza kubaini kuwa katika kitenzi *atamkanya*, kuna kiambishi awali -*ta*- kinachoonesha tendo litafanyika wakati ujao.

Hata hivyo, watahiniwa 192,016 sawa na asilimia 18.97 walichagua vipotoshi: A *Timilifu,* C *Uliopo,* D *Mazoea* na E *Uliopita.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi *timilifu* hawakuelewa kuwa wakati timilifu unatokana na kuwepo kwa kiambishi -me- katika kitenzi. Waliochagua kipotoshi *uliopo* hawakuelewa kuwa wakati uliopo unatokana na kuwepo kwa kiambishi -na- katika kitenzi. Aidha, *waliochagua* kipotoshi *mazoea,* hawakuelewa kuwa neno hilo haliwakilishi wakati ila huwakilisha hali katika sentensi. Vilevile, waliochagua kipotoshi *uliopita* walishindwa kuelewa kuwa wakati *huo huwakilishwa na* kiambishi -li- katika kitenzi kikuu kinachounda sentensi. Watahiniwa walichagua vipotoshi hivyo kwa sababu hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu nyakati mbalimbali katika lugha ya Kiswahili.

**Swali la 17** "Sitakubali kuonewa". Neno "sitakubali" liko katika hali gani?

A Endelevu
B Mazoea
C Timilifu
D Ukanushi
E Uyakinishi.

Swali hili lilitoka katika mada ya Sarufi na lilikuwa linapima ujuzi wa mtahiniwa katika kubaini hali mbalimbali katika sentensi za Kiswahili. Jedwali Na 14 linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.

**Jedwali Na 12: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo**

| **Chaguo** | **A** | **B** | **C** | **D*** | **E** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 190,965 | 119,413 | 102,022 | 561,012 | 28,482 | 9,304 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 18.89 | 11.81 | 10.09 | 55.48 | 2.82 | 0.92 |

Kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa cha wastani kwa sababu watahiniwa 561,012 sawa na asilimia 55.48 walichagua jibu sahihi D *Ukanushi*. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa kuwa sentensi kanushi huundwa na kiambishi awali kanushi *si*- katika kitenzi “**s**itakubali”.

Hata hivyo, watahiniwa 440,882 sawa na asilimia 43.62 walichagua vipotoshi A *Endelevu,* B *Mazoea,* C *Timilifu* na E Uyakinishi. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *endelevu* hawakuelewa kuwa hali hiyo humaanisha: “kuendelea, kusonga mbele bila kikomo” hivyo neno hilo halikuwa jibu sahihi. Waliochagua kipotoshi B *Mazoea,* hawakufahamu kuwa hali ya mazoea ni hali ya kurudia ufanyikaji wa tendo mara kwa mara. Aidha, waliochagua kipotoshi *timilifu* hawakuelewa kuwa timilifu ni wakati unatokana na kuwepo kwa kiambishi -me- katika kitenzi na sio hali, na waliochagua kipotoshi *Uyakinishi* walishindwa kuelewa kuwa ni sentensi zinazoelezea kitu au jambo fulani ila si katika hali ya ukanushi. Watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo hawakuwa na maarifa kuhusu hali mbalimbali zinazotokea katika sentensi za Lugha ya kiswahili.

**Swali la 18:** Mti unakatwa na Ali. Neno “unakatwa” liko katika kauli ipi?

A Kutenda
B Kutendeka
C Kutendea
D Kutendwa
E Kutendewa.

Swali hili lilitoka katika mada ya Sarufi na lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kubaini kauli mbalimbali za vitenzi katika lugha ya

Kiswahili. Jedwali Na 13 linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.

**Jedwali Na 13: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo**

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 85,127 | 103,507 | 38,134 | 630,621 | 146,119 | 7,690 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 8.42 | 10.24 | 3.77 | 62.36 | 14.45 | 0.76 |

Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri kwani watahiniwa 630,621 sawa na asilimia 62.36 walichagua jibu sahihi D *Kutendwa*. Watahiniwa hao waliweza kubaini tabia ya kitenzi ya kupokea viambishi tamati vya kauli mbalimbali baada ya mzizi wa neno -kat- kwa kupachika kiambishi *-w-* cha kauli ya kutendwa pamoja na kiambishi tamati maana - a na kupata neno “unakatwa.”


Watahiniwa 372,887 sawa na asilimia 36.84 walichagua vipotoshi A *Kutenda,* B *Kutendeka,* C *Kutendea na* E *Kutendewa.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi cha *kutenda,* walihusianisha kauli hiyo na sentensi ya swali kuwa “Mti unakatwa na Ali” hivyo walielewa kuwa “Ali anakata mti” ndio maana walichagua kipotoshi hicho. Waliochagua kipotoshi cha *kutendeka,* walishindwa kufahamu maumbo mbalimbali ya viambishi katika utokeaji wa kauli hiyo. Maumbo hayo ni kama vile, -ik-, -ek-, -lek- na -lik-, ambapo kwa muktadha wa swali, kauli hii si jibu sahihi. Aidha, waliochagua kipotoshi cha *kutendea,* walishindwa kuelewa kuwa kauli hiyo huonesha kitendo kimefanywa au kitafanywa kwa manufaa ya mtu au kitu kingine na hutambulika kwa kuwa na maumbo kama vile, -e-, -i-, -li- na –le- katika kitenzi. Pia, waliochagua kipotoshi cha *kutendewa,* walishindwa kuelewa kuwa kauli hiyo huonesha hali ya mtu kufanyiwa jambo na mtu mwingine na hutambulika kwa kuwa na maumbo kama vile, .-iw-, -ew- -lew- na -liw- katika kitenzi. Kwa

jumla, watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu viambishi vya kauli mbalimbali katika lugha ya Kiswahili, na hivyo, kushindwa kubaini kauli sahihi katika swali husika.

**Swali la 19:** "Mtoto alinunuliwa zawadi." Kitenzi "alinunuliwa" kipo katika kauli gani?

A Kutendana
B Kutendewa
C Kutendesha
D Kutenda
E Kutendeka.

Swali hili lilitoka katika mada ya Sarufi na lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kubaini kauli mbalimbali za vitenzi katika lugha ya Kiswahili. Kielelezo Na 6 kinaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa katika kila chaguo.




Kielelezo.Na 6: *Asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo*

Swali hili lilikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwa sababu watahiniwa 835,644 sawa na asilimia 82.64 walichagua jibu sahihi B *Kutendewa*. Watahiniwa hao waliweza kubaini kuwa kauli hiyo huonesha hali ya mtu kufanyiwa jambo na mtu mwingine na

hutambulika kwa kuwa na maumbo mbalimbali kama vile, -iw-, -ew- -lew- na -liw- katika kitenzi. Hivyo, watahiniwa hao walikuwa na maarifa na weledi wa kutosha katika kubaini kauli sahihi katika swali husika.

Watahiniwa 168,581 sawa na asilimia 16.66 walichagua vipotoshi A *Kutendana,* C *Kutendesha,* D *Kutenda* na E *Kutendeka.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi cha *kutendana* walishindwa kuelewa kuwa, kauli hiyo huonesha hali ambayo wahusika hutendana kitendo kile kile, huyu akimtenda yule na wakati huo huo yule akimtenda huyu na hutambulika kwa kuwa na umbo la –an- katika kitenzi. Waliochagua kipotoshi cha *kutendesha,* walishindwa kuelewa kuwa kauli hiyo hutambulika kwa kuwa na maumbo kama vile, -ish-, -esh-, -lish- na -lesh- katika kitenzi.

Aidha, waliochagua kipotoshi cha *kutenda* walishindwa kuelewa kuwa kauli hiyo huagiza kutenda au kufanyika kwa jambo na mara nyingi maumbo yake ni mashina ya vitenzi. Pia, waliochagua kipotoshi cha *kutendeka* walishindwa kufahamu maumbo mbalimbali ya utokeaji wa kauli hiyo, kuwa ni kama vile, -ik-, -ek-, -lek- na –lik- katika kitenzi. Kwa jumla, watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu viambishi vya kauli mbalimbali katika lugha ya Kiswahili, na hivyo, kushindwa kubaini kauli sahihi katika swali husika kuwa ni kutendewa.

**Swali la 20** “Ndizi yake imeliwa na Ngedere”. Wingi wa sentensi hii ni upi?

A Ndizi yake imeliwa na mangedere.

B Ndizi zao zimeliwa na ngedere.

C Ndizi zake zimeliwa na mangedere.

D Mandizi yake yameliwa na mangedere.

E Ndizi zao zimeliwa na mangedere.

Swali hili lilitoka katika mada ya Sarufi na lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kutambua maumbo ya wingi katika sentensi. Jedwali Na 14 linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.

**Jedwali Na 14: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo**

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 29,836 | 702,883 | 196,848 | 30,803 | 44,171 | 5,657 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 2.95 | 69.51 | 19.47 | 3.05 | 4.37 | 0.66 |

Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri kwani watahiniwa 702,883 sawa na asilimia 69.51 waliweza kuchagua jibu sahihi B *Ndizi zao zimeliwa na ngedere.* Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya umoja na wingi katika lugha ya Kiswahili kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya I-ZI ambapo I husimama kwenye umoja na ZI husimama kwenye wingi.

Hata hivyo uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa 301,658 sawa na asilimia 29.83 walichagua vipotoshi A *Ndizi yake imeliwa na mangedere,* C *Ndizi zake zimeliwa na mangedere,* D *Mandizi yake yameliwa na mangedere* na *E Ndizi zao zimeliwa na mangedere.*

Watahiniwa waliochagua kipotoshi *ndizi yake imeliwa na mangedere* hawakuwa na uelewa kuwa katika sentensi hiyo hakuna upatanisho wa kisarufi kwa kuwa kuna maneno yanayoonesha umoja na wingi ndani ya sentensi moja ambapo ni kinyume na kanuni na taratibu katika Lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, maneno “Ndizi yake imeliwa” huonesha hali ya umoja na neno “mangedere” huonesha wingi. Vilevile, katika Lugha ya Kiswahili hakuna wingi wa neno “ngedere”. Watahiniwa

waliochagua kipotoshi *Ndizi zake zimeliwa na mangedere,* walishindwa kuelewa kuwa sentensi hiyo haina upatanisho wa kisarufi kwani, katika kipotoshi hicho kuna neno “*mangedere”* ambapo katika lugha ya Kiswahili hakuna wingi wa neno “ngedere”.

Aidha, waliochagua kipotoshi *Mandizi yake yameliwa na mangedere* walishindwa kuelewa kuwa sentensi hiyo haina upatanisho wa kisarufi kwani katika lugha ya Kiswahili hakuna wingi wa maneno “*ndizi”* na “ngedere” kama yalivyotumika katika kipotoshi husika. Vilevile, kivumishi “yake” kilichotumika katika sentensi hiyo hakikuwa katika hali ya wingi kama yalivyokuwa matakwa ya swali. Pia, waliochagua kipotoshi *Ndizi zao zimeliwa na mangedere* walishindwa kuelewa kuwa neno “mangedere” halikuleta upatanisho wa kisarufi kwa sababu hakuna wingi wa neno “ngedere” katika lugha ya Kiswahili. Hivyo, watahiniwa hao hawakuwa na maarifa juu ya dhana ya upatanisho wa kisarufi katika sentensi hususani katika maumbo ya umoja kuwa wingi.

## 2.2 Sehemu B: Lugha ya Kifasihi

Sehemu hii ilikuwa na maswali kumi (10) ambayo yalimtaka mtahiniwa kutambua matumizi ya lugha ya kifasihi katika methali, nahau, misemo na vitendawili, hususan katika kuelewa maana, miundo na matumizi yake katika lugha ya Kiswahili.

**Swali la 21:** Kamilisha methali hii, “Udongo upate________________.”

A ungali mfinyanzi


B ungali kichanga

C ungali maji

D ingali mapema

E ukiwa na mbolea.

Swali hili lilitoka katika mada ya lugha za kifasihi na lilikuwa na lengo la kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kutambua muundo wa methali za Kiswahili. Kielelezo Na 7 kinaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa katika kila chaguo.




Kielelezo.Na 7: *Asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo*

Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri kwani watahiniwa 838,208 sawa na asilimia 82.89 waliweza kukamilisha methali kwa kuchagua jibu sahihi C *ungali maji*. Watahiniwa hao, walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu muundo sahihi wa methali isemayo “udongo upate ungali maji”. Aidha, walielewa kuwa methali huundwa kwa pande mbili zinazotegemeana kidhima na kimaana.

Hata hivyo, watahiniwa 165,884 sawa na asilimia 16.41 walichagua vipotoshi A *ungali mfinyanzi*, B *ungali kichanga*, D *ingali mapema* na E *ukiwa na mbolea*. Uteuzi wa kipotoshi *ungali mfinyanzi* ulitokana na watahiniwa kuhusisha dhana hiyo na udongo wenye rangi ya kijivu unaonata na hutumika kufinyangia vyungu au matofali. Watahiniwa wengine waliochagua kipotoshi *ungali kichanga* walihusisha na udongo mwepesi unaopatikana pembezoni mwa mto ambao hutumika kujengea nyumba. Aidha,

waliochagua kipotoshi *ingali mapema* walishindwa kuelewa matakwa ya swali kwani neno hilo halina uhusiano kabisa na methali husika. Pia waliochagua kipotoshi *ukiwa na mbolea* walihusianisha methali husika na udongo wenye rutuba. Hivyo, watahiniwa hao hawakuwa na weledi wa kutosha kuhusu miundo ya methali na hivyo kushindwa kukamilisha methali hiyo kwa usahihi.

**Swali la 22:** "________________ ila siku ya idi." Kifungu kipi cha maneno kinakamilisha methali hii?

A Anafunga mchana


B Hatasali

C Hatafaidi pilau

D Mkaidi hafaidi

E Hapati Zawadi

Swali hili lilitoka katika mada ya Lugha za Kifasihi na lilikuwa na lengo la kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kutambua muundo na maana ya methali za Kiswahili. Kielelezo Na. 8 kinaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.




Kielelezo.Na 8: *Asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo*

Kiwango cha ufaulu cha watahiniwa kilikuwa kizuri kwani watahiniwa 801,461 sawa na asilimia 79.26 walichagua jibu sahihi D *Mkaidi hafaidi.* Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha juu ya maana ya methali husika kuwa mtoto mkaidi hafaidi mashauri au nasaha apewazo hadi siku ya Idi anapotambua ubaya wa tabia yake hiyo na kuweza kukamilisha methali husika.

Uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa 202,442 sawa na asilimia 20.04 walichagua vipotoshi A *Anafunga mchana*, *B Hatasali*, *C Hatafaidi pilau* na *E Hapati zawadi.* Waliochagua kipotoshi *anafunga mchana,* walishindwa kuelewa matakwa ya swali kwani walihusianisha na maneno “siku ya Idi” yaliyopo kwenye swali na kufunga mchana kwa waumini wa dini ya kiislamu. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *Hatasali* walihusianisha neno hilo na maneno yaliyopo kwenye sehemu ya swali ambayo ni “siku ya Idi”. Kuwa mtu huyo hatasali mpaka siku ya Idi.

Aidha, waliochagua kipotoshi *hatafaidi pilau* walihusianisha sikukuu ya Idi na ulaji wa pilau. Vilevile, waliochagua kipotoshi *hupata zawadi* walihusianisha sikukuu ya Idi na kupata zawadi kwa kuwa watu hupeana zawadi mbalimbali siku hiyo. Hivyo watahiniwa hao walishindwa kuwa wadadisi wa kuelewa pande mbili za methali “Mkaidi hafaidi ila siku ya Idi” hivyo, kuchagua vipotoshi ambavyo havina uhusiano na swali.

**Swali la 23:** “Mla nawe hafi nawe ila mzaliwa nawe.” Methali hii inahusiana na ipi kati ya zifuatazo?

A Jembe halimtupi mtu

B Baada ya dhiki faraja

C Damu ni nzito kuliko maji

D Penye urembo ndipo penye ulimbo

E Kila mtoto na koja lake.

Swali hili lilitoka katika mada ya Lugha ya Kifasihi na lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kutambua methali zenye maana sawa katika Lgha ya Kiswahili. Jedwali Na. 15 linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.

**Jedwali Na.19: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo**

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 132,886 | 102,791 | 528,157 | 123,185 | 113,789 | 10,390 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 13.14 | 10.17 | 52.23 | 12.18 | 11.25 | 1.03 |

Kiwango cha ufaulu cha watahiniwa kilikuwa cha wastani kwani watahiniwa 528,157 sawa na asilimia 52.23 walichagua jibu sahihi C Damu ni nzito kuliko maji. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha juu ya maana ya methali “Mla nawe hafi nawe ila mzaliwa nawe” kuwa uhusiano wa kidamu ni muhimu sana kwani ndio unaoweza kutufaa pale tunapopata matatizo. Hivyo, kuweza kubainisha methali husika katika swali.

Hata hivyo, watahiniwa 472,651 sawa na asilimia 46.77 walichagua vipotoshi A *Jembe halimtupi mtu,* B *Baada ya dhiki faraja,* D *Penye urembo ndipo penye ulimbo* na E *Kila mtoto na koja lake*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *Jembe halimtupi mtu* walishindwa kuelewa maana ya methali hiyo kuwa; mkulima anayelima kwa bidii hakosi kuambulia kitu. Waliochagua kipotoshi *Baada ya dhiki faraja* Walishindwa kuelewa kuwa methali hiyo inamaanisha kuwa tunapopatwa na shida tunapaswa kupambana na shida hizo kwa kuwa baadaye tutapata raha.

Aidha, watahiniwa wengine walichagua kipotoshi *Penye urembo ndipo penye ulimbo*, ikiwa na maana ya tusikiendee kitu fulani kwa

pupa kwa kuwa huvutia kwa sababu huenda kikawa na madhara fulani. Vilevile, uteuzi wa kipotoshi *kila mtoto na koja lake* haukuwa sahihi kwani kila mtu huwa na vitu vyake avipendavyo. Kwa ujumla watahiniwa hao walishindwa kuelewa maana ya methali hizo na kuwa hazina uhusiano kabisa na methali “Mla nawe hafi nawe ila mzaliwa nawe” yenye maana kuwa uhusiano wa kidamu ni muhimu sana kwani ndio unaoweza kutufaa pale tunapopata matatizo.

**Swali la 24** “Hana adabu wala staha kwa watu.” Jibu la kitendawili hiki ni lipi?

A Kinyesi
B kamasi
C Jasho
D Utelezi
E Pombe.

Swali hili lilitoka katika mada ya Lugha ya Kifasihi na lilikuwa linapima ujuzi wa mtahiniwa katika kutegua vitendawili. Jedwali Na. 20 linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.

**Jedwali Na. 16: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo**

| **Chaguo** | **A** | **B** | **C** | **D*** | **E** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 135,395 | 96,424 | 54,022 | 650,058 | 67,335 | 7,964 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 13.39 | 9.54 | 5.34 | 64.29 | 6.66 | 0.79 |

Kiwango cha ufaulu cha watahiniwa kilikuwa kizuri kwa sababu watahiniwa 650,058 sawa na asilimia 64.29 walichagua jibu sahihi D *Utelezi* hivyo kutegua kitendawili husika kwa usahihi. Watahiniwa hao waliweza kubaini kuwa utelezi huweza kumuumbua mtu mbele za watu. Hii inathibitisha kuwa watahiniwa hao walikuwa na maarifa

ya kutosha kuhusu maana ya fumbo lililojengwa katika kitendawili hicho.

Watahiniwa 353,176 sawa na asilimia 34.92 walichagua vipotoshi A *Kinyesi,* B *Kamasi,* C *Jasho* na E *Pombe.* Watahiniwa waliochagua hivyo, walikuwa na dhana kuwa, vyote hivyo ni uchafu unaotoka katika mwili wa binadamu, hivyo uchafu huo ukitoka mbele za watu, mtu huyo anakuwa hana staha kwa watu hivyo kuhusianisha na kitendawili husika. Pia watahiniwa waliochagua kipotoshi *pombe* walikuwa na mtazamo kuwa, kwa kuwa pombe ni kinywaji kinacholewesha, mtu akilewa sana anaweza kutenda matendo mabaya ambayo humfanya kukosa adabu na staha kwa watu. Hivyo, watahiniwa hao, hawakuwa na maarifa ya kufumbua mafumbo yaliyojengwa katika kitendawili, hatimaye kushindwa kutegua kitendawili "Hana adabu wala staha kwa watu".

**Swali la 25:** "Mwavuli wa nyikani haukingi mvua." Jibu la kitendawili hiki ni lipi?

A Mgomba

B Mpapai

C Uyoga

D Mnyonyo

E Mfenesi.

Swali hili lilitoka katika mada ya Lugha ya Kifasihi na lilikuwa linapima ujuzi wa mtahiniwa katika kutegua vitendawili. Jedwali Na. 17 linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.

**Jedwali Na. 17: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo**

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 99,554 | 79,275 | 734,193 | 47,333 | 41,328 | 9,515 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 9.85 | 7.84 | 72.61 | 4.68 | 4.09 | 0.94 |

Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri kwani watahiniwa 734,193 sawa na asilimia 72.61 walichagua jibu sahihi C *Uyoga* (mmea wenye umbo la mwavuli wa jamii ya ukungu unaoota kwenye mimea na miti iliyooza au kwenye samadi na hutumiwa kama mboga). Huu ni uthibitisho kuwa watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maana ya fumbo lililojengwa katika kitendawili hivyo kutegua kwa usahihi kuwa ni *uyoga*.

Hata hivyo, watahiniwa 267,490 sawa na asilimia 26.45 walichagua vipotoshi A *Mgomba,* B *Mpapai,* D *Mnyonyo* na E *Mfenesi.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi *Mgomba* walikuwa na dhana isiyo sahihi kuwa *Mgomba* una umbo linalofanana na mwavuli na hupatikana hata mazingira ya nyumbani na si nyikani tu. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *mpapai* walishindwa kuelewa kuwa mmea huo hauna uhusiano na swali husika kiumbo wala kimaana. Aidha, waliochagua kipotoshi *mnyonyo* walikuwa na dhana isiyo sahihi kuwa neno hilo lina umbo la mwavuli na hupatikana nyikani tu. Pia uteuzi wa kipotoshi *Mfenesi* unaonesha kuwa watahiniwa hao walihusianisha umbo la mmea huo na swali husika. Kwa ujumla watahiniwa walikosa maarifa ya kufumbua fumbo lililojengwa katika kitendawili, hivyo, kushindwa kubaini kuwa kati ya mimea mitano iliyotajwa kwenye chaguzi, uyoga pekee ndio mmea wenye umbile linalofanana na mwavuli.

**Swali la 26:** "Akibeba watoto wake hawezi kuwashusha." Jibu la kitendawili hiki ni lipi?

A Mzaituni


B Mhindi

C Mchungwa

D Mwembe

E Mpera.

Swali hili lilitoka katika mada ya Lugha ya Kifasihi na lilikuwa linapima ujuzi wa mtahiniwa katika kutegua vitendawili. Kielelezo Na. 9 kinaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa katika kila chaguo.




Kielelezo Na 9*: Asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo*

Kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri kwa sababu watahiniwa 766,195 sawa na asilimia 75.77 walichagua jibu sahihi B *Mhindi.* Watahiniwa hao waliweza kubaini kuwa mhindi ni mmea ambao hubeba mazao (mahindi) ambayo yakikomaa lazima yachumwe tofauti na mimea mingine ambayo matunda yake hudondoka yenyewe baada ya kukomaa. Huu ni uthibitisho kuwa watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maana ya fumbo lililojengwa katika kitendawili husika.

Hata hivyo uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa 236,610 sawa na asilimia 23.40 walichagua vipotoshi A *Mzaituni,* C *Mchungwa* D *Mwembe* na E *Mpera.* Watahiniwa waliochagua vipotoshi *mzaituni, Mchungwa, Mwembe* na *Mpera* walishindwa kuelewa kuwa vipotoshi vyote hivyo ni mimea ambayo hubeba mazao (matunda) ambayo yakikomaa hudondoka yenyewe bila kuchumwa. Uteuzi wa vipotoshi hivyo unaonesha kuwa, watahiniwa hao hawakufahamu kuwa maumbo ya vitu vilivyotajwa hayasadifu umbo lililofichwa katika kitendawili husika.

**Swali la 27:** "Babu huanika sembe usiku, asubuhi huiondoa." Jibu la kitendawili hiki ni lipi?

A Mvua

B Giza

C Mwezi

D Umande

E Mawingu.

Swali hili lilitoka katika mada ya Lugha ya Kifasihi na lilikuwa linapima ujuzi wa watahiniwa katika kutegua vitendawili. Jedwali Na 18 linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.

**Jedwali Na. 18: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo**

| **Chaguo** | **A** | **B** | **C** | **D*** | **E** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 24,831 | 308,295 | 420,390 | 200,576 | 49,099 | 8,007 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 2.46 | 30.49 | 41.57 | 19.84 | 4.86 | 0.79 |

Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa hafifu kwani watahiniwa 802,615 sawa na asilimia 79.37 walichagua Vipotoshi A *Mvua,* B *Giza,* C *Mwezi* na E *Mawingu.* Watahiniwa waliochagua

kipotoshi *mvua* walihusianisha sembe na matone matone meupe ya mvua. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *giza,* walihusianisha giza na neno “usiku” kama lilivyotumika katika swali husika, hivyo kuona kuwa kipotoshi hicho ndio jibu sahihi. Uteuzi wa kipotoshi *mwezi,* unatokana na watahiniwa kuona kuwa mwezi ni mweupe wenye umbile la duara na unaonekana sana usiku na asubuhi hauonekani kirahisi kwa kutoa mwanga hivyo walihusianisha kipotoshi *mwezi* na neno sembe katika kitendawili husika. Aidha, waliochagua kipotoshi *mawingu*, walihusianisha rangi nyeupe inayoonekana kwenye mawingu na maneno “huanika sembe usiku” yaliyoko katika swali husika hivyo kuona kuwa kipotoshi hicho ni jibu sahihi. Kwa ujmla, watahiniwa hao walikosa maarifa ya udadisi katika vipotoshi hivyo visivyo na uhusiano wa moja kwa moja na kitendawili husika hivyo kushindwa kufumbua mafumbo yaliyojengwa katika kitendawili hicho.

Vilevile, watahiniwa 200,576 sawa na asilimia 19.84 walichagua jibu sahihi D *Umande*. Watahiniwa hao waliweza kufumbua fumbo lililojengwa katika kitendawili “Babu huanika sembe usiku, asubuhi huiondoa.” kwa kuwa umande hutokea usiku na asubuhi hutoweka. Hivyo, watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maana ya kitendawili husika.

**Swali la 28:** “Unga mkono.” Maana ya nahau hii ni ipi?

A Kushikana mkono

B Ongozana


C Kubaliana

D Fuatana

E Tembeleana.

Swali hili lilitoka katika mada ya Lugha ya Kifasihi na lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kutambua maana za nahau

mbalimbali katika lugha ya Kiswahili. Kielelezo Na. 10 kinaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa katika kila chaguo.




Kielelezo Na 10*: Asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo*

Kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri kwa kuwa watahiniwa 846,896 sawa na asilimia 83.75 walichagua jibu sahihi C *Kubaliana.* Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maana ya nahau "Unga mkono" kuwa ni hali ya kukubaliana na hoja au jambo lisemwalo. Hivyo, waliweza kuchagua jibu sahihi lenye maana ya nahau husika.

Aidha, watahiniwa 155,590 sawa na asilimia 15.39 walichagua vipotoshi A *Kushikana mkono*, B *Ongozana*, D *Fuatana* na E *Tembeleana*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *kushikana mkono* walishindwa kuelewa maana ya neno hilo kuwa ni tia kitu au mtu mwingine mkononi, kamatana. Hivyo "kushikana mkono" haliendani na maana ya nahau husika. Vilevile, waliochagua kipotoshi *ongozana* na *fuatana* walishindwa kuelewa maana ya maneno hayo kuwa ni *tembea pamoja ikiwa mmoja mbele mwingine nyuma*. Pia, waliochagua kipotoshi *tembeleana* walishindwa kuelewa kuwa neno hilo lina maana ya mtu mmoja anamtembelea mwenzake na

mwenzake anafanya hivyo hivyo. Kwa ujumla, watahiniwa hao walikuwa hawana maarifa ya kutosha kuhusu maana ya nahau “unga mkono” katika lugha ya Kiswahili.

**Swali la 29:** Ni nahau ipi kati ya zifuatazo inadhihirisha hali ya kumsema mtu kwa mafumbo ili asitambue?

A Kumpiga vijembe

B Kumpiga kinagaubaga

C Kumsema kimasomaso

D Kumsema kisiasa.

E Kumsema kwa kumjuza.

Swali hili lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika matumizi ya misemo. Jedwali Na. 19 linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.

**Jedwali Na 19: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo**

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 393,511 | 184,446 | 176,092 | 184,195 | 60,832 | 12,122 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 38.92 | 18.24 | 17.41 | 18.22 | 6.02 | 1.20 |

Kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa hafifu kwani watahiniwa 605,565 sawa na asilimia 41.6 walichagua vipotoshi B *Kumpiga kinagaubaga,* C *Kumsema kimasomaso,* D *Kumsema kisiasa* na E *Kumsema kwa kumjuza.* Watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo walishindwa kuelewa kuwa vipotoshi hivyo vina maana inayofafana kuwa: ni kumsema mtu kwa uwazi bila kumficha au kumumunya maneno hivyo ni tofauti na nahau “kumpiga vijembe” yenye maana ya kumsema mtu kwa mafumbo ili asitambue. Uteuzi wa vipotoshi hivyo ulitokana na watahiniwa hao

kushindwa kuelewa maana ya nahau mbalimbali za Lugha ya Kiswahili.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 393,511 sawa na asilimia 38.92 walichagua jibu sahihi A *kumpiga vijembe* likiwa na maana ya *kumsema mtu kwa mafumbo ili asitambue*. Hii inaonesha kuwa watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maana ya nahau "*kumpiga vijembe*".

**Swali la 30:** "Nikipata wasaa nitajitahidi kukutupia jicho." Usemi "kukutupia jicho" una maana gani?

A Kukusikiliza
B Kukuletea fedha
C Kukupa miwani
D Kukuona
E Kukupima macho.

Swali hili lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kutambua maana ya semi mbalimbali. Jedwali Na 20 linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.

**Jedwali Na. 20: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo**

| **Chaguo** | **A** | **B** | **C** | **D*** | **E** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 98,086 | 80,313 | 42,648 | 749,659 | 29,495 | 10,997 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 9.70 | 7.94 | 4.22 | 74.14 | 2.92 | 1.09 |

Kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri kwa sababu watahiniwa 749,659 sawa na asilimia 74.14 walijibu swali hili kwa usahihi kwani waliweza kubaini maana ya usemi kwa kuchagua jibu sahihi A *Kukuona.* Watahiniwa hao, walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maana ya usemi "kukutupia jicho" kuwa

ni  kitendo cha kumuona mtu kwa lengo la kumsalimia au kumjulia hali. Aidha, watahiniwa hao waliweza kuelewa lugha ya picha inayotumika katika usemi huo na kuweza kutafsiri maana hiyo katika lugha ya kawaida.

Hata hivyo, watahiniwa 250,542 sawa na asilimia 24.76 walichagua vipotoshi A *Kukusikiliza,* B *Kukuletea fedha,* C *Kukupa miwani na E Kukupima macho,* kutokana na kukosa uelewa wa maana ya usemi husika. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *kukusikiliza* walishindwa kuelewa kuwa neno hilo lina maana ya kutega sikio ili usikie sauti inayosemwa au kusikika ambapo ni kinyume cha usemi "kukutupia jicho." Vilevile, Waliochagua kipotoshi *kukuletea fedha*, walishindwa kuelewa maana ya neno hilo kuwa ni kufikisha fedha kwa mtu anayetakiwa.

Aidha, waliochagua kipotoshi *kukupa miwani* walishindwa kuelewa maana yake kuwa ni kupewa miwani. na waliochagua kipotoshi *kukupima macho* walishindwa kuelewa kuwa ni kitendo cha kuchunguza macho kwa kutumia kipimo kinachostahili. Hivyo, watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo, hawakuwa na maarifa ya kutosha katika kutafsiri lugha ya picha inayotumika katika semi mbalimbali, hivyo kushindwa kuchagua maana sahihi.

## 2.3 Sehemu C: Ushairi

Sehemu hii ilikuwa na maswali sita (6) ambayo yalimtaka mtahiniwa kusoma kwa makini shairi na kutumia maarifa aliyojifunza katika ushairi kujibu maswali yaliyotokana na shairi hilo. Watahiniwa walipewa shairi lifuatalo:

*Kuwaza na kuwazua, matukio mbalimbali,*
*Ndivyo akili yakua, pungufu kuwa kamili,*
*Asojua akajua, kwa lile ama kwa hili,*
*Lau ukipuuzia, katu hutofika mbali.*

*Kusoma na kuchambua, vitabu na mafaili,*
*Mambo ukapambanua, ya uwongo na ukweli,*
*Hapo hatokusumbua, kila aliye jahili,*
*Lau ukipuuzia, katu hutofika mbali.*

*Kupanga na kupangua, mikakati ya halali,*
*Utaweza kubagua, lilo jema na batili,*
*Jema utalichukua, baya utaweka mbali,*
*Lau ukipuuzia, katu hutofika mbali.*

**Swali la 31:** Kichwa kinachofaa kwa shairi hili ni kipi?

A Umuhimu wa Elimu
B Kusoma na kuchambua
C Kupanga na kupangua
D Katu hutofika mbali
E Asojua akajua.

Swali hili lilitoka katika mada ya Ushairi na lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kutambua kichwa cha shairi alilolisoma. Jedwali Na. 21 linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa katika kila chaguo.

**Jedwali Na. 21: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo**

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 603,252 | 160,512 | 91,728 | 78,194 | 64,119 | 13,393 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 59.66 | 15.87 | 9.07 | 7.73 | 6.34 | 1.32 |

Kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa cha wastani kwa kuwa watahiniwa 603,252 sawa na asilimia 59.66 walichagua jibu sahihi A *Umuhimu wa elimu.* Hii inaonesha kuwa watahiniwa wa kundi hili walitambua wazo kuu ambalo linajirudia katika kila ubeti wa shairi. Uwezo huo unatokana na kusoma kwa ufahamu, hivyo kubaini kichwa cha shairi hilo kwa usahihi.

Hata hivyo, jumla ya watahiniwa 394,553 sawa na asilimia 39.02 walichagua vipotoshi B *Kusoma na kuchambua,* C *Kupanga na kupangua,* D *Katu hutofika mbali* na *E Asojua akajua.* Watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo walishindwa kuelewa kuwa, kichwa cha shairi kinatokana na wazo kuu ambalo linajirudia katika kila ubeti wa shairi kuanzia mwanzo hadi mwisho badala ya kuchukuwa maneno fulani kutoka katika shairi husika. Kwa mfano, waliochagua kipotoshi *kusoma na kuchambua* ulisababishwa na watahiniwa kuona mshororo usemao “kusoma na kuchambua, vitabu na mafaili” katika ubeti wa pili ambao ulikuwa unasisitiza umuhimu wa kusoma vitabu na mafaili ili kuweza kupambanua ukweli na uwongo. Vilevile, watahiniwa waliochagua kipotoshi *kupanga na kupangua* walivutiwa na ubeti wa tatu wenye mshororo usemao “kupanga na kupangua, mikakati ya halali” ambalo siyo jibu sahihi kwani shairi linahimiza umuhimu wa Elimu.

Aidha, waliochagua kipotoshi *katu hutofika mbali* ulisababishwa na watahiniwa kuona neno hilo katika kiitikio cha shairi. Hata hivyo, kiitikio hicho kilikuwa kina mtahadharisha msomaji asipuuzie Elimu kwani ni muhimu sana katika maisha ya binadamu. Pia, uteuzi wa kipotoshi *asojua akajua* ulitokana na watahiniwa kuhusisha ujumbe uliopo katika ubeti wa kwanza na maneno *asojua akajua* yaliyopo katika mstari wa tatu wa ubeti huo. Kwa jumla, uteuzi wa vipotoshi

hivyo hauendani na kichwa cha shairi kwani baadhi ya maneno hayo yalijitokeza katika sehemu chache za shairi.

**Swali la 32:** Vina vya kati na vya mwisho katika mistari ya ubeti wa tatu ni vipi?

A u na li


B ku na li

C a na li

D ku na u

E ta na we.

Swali hili lilitoka katika mada ya Ushairi na lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kuhusu kanuni za utunzi wa mashairi ya kimapokeo katika lugha ya Kiswahili. Kielelezo Na. 11 kinaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.




Kielelezo Na 11*: Asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo*

Kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri kwani watahiniwa 850,835 sawa na asilimia 84.14 waliweza kuchagua jibu sahihi C *a* na *li* ambazo ni silabi za mwisho katika

kila kipande cha ubeti wa tatu wa shairi hilo. Hii inathibitisha kuwa, watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu muundo wa shairi, hivyo kubaini vina vya kati na vya mwisho katika ubeti husika kwa usahihi.

Uchambuzi unaonesha kuwa, watahiniwa 150,341 sawa na asilimia 14.84 walichagua vipotoshi A *u* na *li,* B *ku* na *li,* D *ku* na *u*, na E *ta* na *we.* Watahiniwa wa kundi hili walikosa maarifa juu ya dhana ya vina katika shairi kuwa ni silabi ya kati na ya mwisho katika mstari wa shairi. Hivyo, walichagua silabi ambazo zimetokea katika shairi kwenye nafasi ambazo haziwezi kuwa na sifa ya kuwa vina vya kati wala vya mwisho kwa mujibu wa kanuni za muundo wa shairi katika lugha ya Kiswahili. Uchaguzi wa vipotoshi hivyo unathibitisha kuwa watahiniwa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya vina vya kati na mwisho katika ubeti wa shairi.

**Swali la 33:** Jumla ya silabi kumi na sita katika kila mstari wa shairi huitwaje?

A Ubeti

B Mizani

C Vina

D Silabi

E Mshororo.

Swali hili lilitoka katika mada ya Ushairi na lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kuhusu muundo wa shairi. Jedwali Na. 22 linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.

**Jedwali Na. 22: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo**

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 53,080 | 604,847 | 60,115 | 42,045 | 241,434 | 9,677 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 5.25 | 59.81 | 5.94 | 4.16 | 23.88 | 0.96 |

Kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa cha wastani kwani watahiniwa 604,847 sawa na asilimia 59.81 walichagua jibu sahihi B *Mizani.* Huu ni uthibitisho kuwa watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha juu ya kanuni za uundaji wa mashairi hivyo waliweza kubaini kuwa *mizani* ni idadi ya silabi katika mshororo wa shairi.

Hata hivyo, watahiniwa 396,674 sawa na asilimia 39.23 walishindwa kujua kuwa Jumla ya silabi kumi na sita katika kila mstari wa shairi huitwa mizani. Hivyo, walichagua vipotoshi A *Ubeti,* C *Vina,* D *Silabi na* E *Mshororo.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi *ubeti* hawakuelewa kuwa, neno hilo si jumla ya silabi kumi na sita katika kila mstari wa shairi bali ni aya zinazounda shairi ambapo huweza kuundwa na mistari mitatu au minne. Vilevile, waliochagua kipotoshi *Vina*, walishindwa kuelewa kuwa vina ni silabi ya kati na ya mwisho katika kila mshororo wa shairi.

Pia, watahiniwa waliochagua kipotoshi *silabi*, walishindwa kuelewa kuwa silabi ni sehemu ya neno ambalo hutamkwa mara moja na kwa pamoja kama fungu moja la sauti. Vilevile, waliochagua kipotoshi *mshororo,* walishindwa kuelewa maana ya neno hilo kuwa ni mstari wowote katika ubeti wa shairi. Hivyo, watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu "mizani" ambayo ni idadi ya silabi katika mshororo wa shairi.

**Swali la 34**: Shairi hili lina mizani ngapi?

A Nane

B Kumi

C Nne

D Kumi na mbili

E Kumi na sita.

Swali lilitoka katika mada ya Ushairi na lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kuhusu muundo wa shairi katika lugha ya Kiswahili. Jedwali Na. 23 linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.

**Jedwali Na. 23 Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo**

| **Chaguo** | **A** | **B** | **C** | **D** | **E*** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 40,674 | 24,825 | 52,571 | 147,141 | 735,783 | 10204 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 4.02 | 2.46 | 5.20 | 14.55 | 72.76 | 1.01 |

Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri kwa kuwa watahiniwa 735,783 sawa na asilimia 72.76 waliweza kuchagua jibu sahihi *E kumi na sita*. Watahiniwa hao walifahamu kuwa mizani ni jumla ya silabi katika mshororo (mstari) wa shairi.


Hata hivyo, watahiniwa 265,211 sawa na asilimia 26.23 walichagua vipotoshi A *Nane*, B *Kumi*, C *Nne* na D *Kumi na mbili*. Hii inaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mizani katika mashairi. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *nane*, walielewa kuwa mizani ni idadi ya silabi katika kipande kimoja cha mstari wa shairi badala ya idadi ya silabi kwa mstari mzima. Vilevile, uteuzi wa kipotoshi *kumi* ulitokana na watahiniwa kushindwa kufahamu maana ya mizani kuwa ni jumla ya silabi katika mshororo (mstari) wa shairi hivyo kushindwa kuchagua jibu sahihi. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *nne*, walihesabu idadi ya mistari katika ubeti na kudhani kuwa ndio mizani. Watahiniwa wengine walichagua kipotoshi *kumi na mbili* kwa kuwa walihesabu idadi ya mistari katika shairi zima lenye beti tatu na kudhani kuwa mistari hiyo ndio mizani. Uteuzi wa vipotoshi hivyo unaonesha kuwa

watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu muundo wa shairi hususan katika dhana ya mizani.

**Swali la 35:** Kituo kilichotumika katika shairi hili ni kipi?

A Jema utalichukua, baya utaweka mbali,
B Kuwaza na kuwazua, matukio mbalimbali,
C Hapo hatokusumbua, kila aliye jahili,
D Lau ukipuuzia, katu hutofika mbali
E Kupanga na kupangua, mikakati ya halali,

Swali lilitoka katika mada ya Ushairi na lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kuhusu muundo wa shairi katika lugha ya Kiswahili. Kielelezo Na. 12 kinaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.



Kielelezo Na 12*: Asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.*

Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri kwani watahiniwa 826,513 sawa na asilimia 81.74 waliweza kuchagua jibu sahihi *D Lau ukipuuzia, katu hutofika mbali*. Watahiniwa hao

walibahini kuwa kituo ni mshororo wa mwisho kwenye ubeti wa shairi unaojirudiarudia katika kila ubeti.

Aidha, watahiniwa 174,983 sawa na asilimia 17.30 walichagua vipotoshi A *Jema utalichukua*, *baya utaweka mbali,* B *Kuwaza na kuwazua*, *matukio mbalimbali,* C *Hapo hatokusumbua, kila aliye jahili* na E *Kupanga na kupangua*, mikakati ya halali. Watahiniwa wa kundi hili hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu dhana ya "kituo" katika ushairi kwani walichagua vipotoshi ambavyo maneno yake ni mistari iliyojitokeza tu katika beti mbalimbali badala ya mstari wa mwisho unaojirudiarudia. Kwa mfano, waliochagua kipotoshi *jema utalichukua*, *baya utaweka mbali,* ni maneno yaliyopo katika mstari wa tatu katika ubeti wa tatu.

Hata hivyo, waliochagua kipotoshi *kuwaza na kuwazua*, *matukio mbalimbali,* walichaga maneno yaliyopo katika mstari wa kwanza katika beti wa kwanza. Vilevile, waliochagua kipotoshi *hapo hatokusumbua, kila aliye jahili* walishindwa kubaini kuwa maneno hayo yapo ubeti wa pili mstari wa tatu na si mstari wa mwisho wa ubeti huo. Waliochagua *kupanga na kupangua*, *mikakati ya halali* walishindwa kufahamu kuwa maneno hayo yapo ubeti wa tatu mstari wa kwanza. Hii, inadhihirisha kuwa, watahiniwa hao hawakuwa na maarifa na ufahamu wa kutosha kuelewa dhana ya kituo kuwa ni mstari wa mwisho katika kila beti unaojirudiarudia.

**Swali la 36:** Neno "jahili" kama lilivyotumika katika ubeti wa pili lina maana gani?

A Mjanja

B Mpole

C Mjinga

D Mwizi

E Hasidi.

Swali hili lilitoka katika mada ya Ushairi na lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kutambua maana ya msamiati uliotumika katika shairi. Jedwali Na 24 linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.

**Jedwali Na. 24: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo**

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 425,976 | 101,219 | 296,196 | 96,372 | 77,314 | 14,121 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 42.13 | 10.01 | 29.29 | 9.53 | 7.65 | 1.40 |

Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa hafifu kwani watahiniwa 700,881 sawa na asilimia 69.31 walichagua vipotoshi A *Mjanja,* B *Mpole,* D *Mwizi* na E *Hasidi*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *mjanja* hawakuelewa kuwa maana ya neno hilo ni mtu laghai aliyejaa hila katika kufanya jambo. Maana hiyo inakinzana na maana ya “jahili” ambayo ni mtu mwenye uwezo mdogo wa kuelewa mambo kama ulivyotumika katika shairi.

Pia, watahiniwa waliochagua kipotoshi *mpole,* hawakutambua kuwa, neno mpole ni mtu ambaye ni mtulivu na ambaye hafanyi vurugu au ghasia yoyote kwa mtu. Aidha, uteuzi wa kipotoshi *mwizi* ulitokana na watahiniwa kutokuelewa maana ya neno hilo kuwa ni mtu mwenye tabia ya kuchukua mali ya mtu mwingine bila ruhusa. Pia, waliochagua kipotoshi *hasidi* hawakuelewa kuwa ni mtu mwenye wivu, asiyependa mafanikio ya wenzake, mchoyo. Kutokana na uchaguzi wa vipotoshi hivyo inadhihirisha kuwa, watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kubaini maana ya msamiati “jahili” ambao unamaanisha mtu mwenye uwezo mdogo wa kuelewa mambo kama ulivyotumika katika shairi.

Hata hivyo, watahiniwa 296,196 sawa na asilimia 29.29 ndio walioweza kuchagua jibu C *Mjinga* ikiwa na maana ya mtu asiye na uelewa wa jambo fulani au mbumbumbu. Watahiniwa hao waliweza kuhusianisha msamiati “jahili” na neno *mjinga* ambalo linabeba maana ya msingi ya msamiati huo kama lilivyotumika katika shairi.

## 2.4 Sehemu D: Utungaji

Sehemu hii ililenga kupima uwezo wa watahiniwa wa kupanga mawazo katika mtiririko wenye mantiki. Katika sehemu hii watahiniwa walipewa habari yenye sentensi nne (4) zilizoandikwa bila mtiririko sahihi na walitakiwa kuzipanga ili ziwe na mtiririko wenye mantiki kwa kuzipa herufi A, B, C na D.

37. Hivyo huwa ni mzigo mkubwa kwa familia na jamii kwa ujumla.
38. Unywaji wa pombe husababisha madhara makubwa.
39. Watu waliotawaliwa na pombe hutumia pesa na muda mwingi kwenye pombe.
40. Wengine pombe huwasababishia magonjwa mbalimbali.

**Swali la 37:** Hivyo huwa ni mzigo mkubwa kwa familia na jamii kwa ujumla.

Swali lilitoka katika mada ya Utungaji na lilimtaka mtahiniwa kupanga sentensi namba 37 kwa kuandika herufi moja wapo kati ya A, B, C na D katika mtiririko unaoleta mantiki ili kuunda kifungu cha habari chenye maana. Jedwali Na. 25 linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.

**Jedwali Na. 25: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo**

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 44,157 | 145,265 | 132,779 | 655,720 | 23,753 | 9,524 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 4.37 | 14.37 | 13.13 | 64.85 | 2.35 | 0.94 |

Kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri kwani watahiniwa 655,720 sawa na asilimia 64,85 walipanga sentensi hii katika mtiririko kwa kuandika kwa usahihi herufi D ili kuunda habari fupi yenye mantiki. Watahiniwa hao, waliweza kuelewa kuwa , sentensi hiyo ni sentensi ya mwisho kutokana na viashiria vya maneno kama vile, "hivyo" na vilevile ni sentensi inayohitimisha kifungu cha habari. Kwa ujumla, upangaji huu unaonesha kuwa, watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu kupanga mawazo katika mtiririko wenye mantiki na kuunda kifungu cha habari.

Hata hivyo, watahiniwa 23,753 sawa na asilimia 2.35 waliandika herufi E isiyokuwa na sentensi yoyote kati ya sentensi zilizokuwa katika habari kutokana na kutoelewa matakwa ya swali kwani walitakiwa kuzipanga sentensi hizo katika herufi A, B, C na D katika mtiririko unaoleta mantiki ili kuunda kifungu cha habari chenye maana.

**Swali la 38:** Unywaji wa pombe husababisha madhara makubwa.

Swali lilitoka katika mada ya Utungaji na lilimtaka mtahiniwa kupanga sentensi namba 38 kwa kuandika herufi moja wapo kati ya A, B, C na D katika mtiririko unaoleta mantiki ili kuunda kifungu cha habari chenye maana. Jedwali Na. 26 linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.

**Jedwali Na. 26: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo**

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 678,854 | 149,188 | 96,493 | 67,676 | 10,808 | 4,090 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 67.13 | 14.75 | 9.54 | 6.69 | 1.07 | 0.81 |

Kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri ambapo watahiniwa 678,854 sawa na asilimia 67.13 walipanga sentensi hii katika mtiririko kwa kuandika kwa usahihi herufi A ili kuunda habari fupi yenye mantiki. Watahiniwa hao, waliweza kuelewa kuwa, sentensi hiyo ni sentensi ya kwanza kwa sababu imeanza kwa kuelezea wazo kuu la habari husika kuhusu madhara ya unywaji wa pombe. Upangaji huu unaonesha kuwa, watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Utungaji hususani katika kupanga mawazo yenye mtiririko unaoleta mantiki ili kuunda kifungu cha habari.

Hata hivyo, watahiniwa 10,808 sawa na asilimia 1.07 walichagua E isiyokuwa na sentensi yoyote kati ya sentensi zilizokuwa katika habari kutokana na kukosa ujuzi wa kutunga habari fupi yenye mantiki na kutokuelewa matakwa ya swali.

**Swali la 39:** Watu waliotawaliwa na pombe hutumia pesa na muda mwingi kwenye pombe.

Swali lilitoka katika mada ya Utungaji na lilimtaka mtahiniwa kupanga sentensi namba 39 kwa kuandika herufi moja wapo kati ya A, B, C na D katika mtiririko unaoleta mantiki ili kuunda kifungu cha habari chenye maana. Jedwali Na. 27 linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.

**Jedwali Na. 27: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo**

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 213,119 | 459,686 | 224,905 | 92,828 | 12,285 | 8,375 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 21.08 | 45.46 | 22.24 | 9.18 | 1.21 | 0.83 |

Kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa cha wastani kwani watahiniwa 459,686 sawa na asilimia 45.46 walipanga sentensi hii katika mtiririko kwa kuandika kwa usahihi herufi B ili kuunda habari fupi yenye mantiki. Watahiniwa hao waliweza kubaini kuwa sentensi ya 38 iliyoandikwa kuwa “unywaji wa pombe husababisha madhara makubwa” inafuatiwa na sentensi ya 39 inayoelezea madhara hayo na hivyo inapaswa kuwa sentensi ya pili “B”. Upangaji huu unaonesha kuwa watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu upangaji wa matukio katika mtiririko wenye mantiki na kuweza kuunda kifungu cha habari.

Hata hivyo, watahiniwa 12,285 sawa na asilimia 1.21 walichagua herufi E isiyokuwa na sentensi yoyote kati ya sentensi zilizokuwa katika habari kutokana na kukosa ujuzi wa kutunga habari fupi yenye mantiki na kutozingatia matakwa ya swali husika.

**Swali la 40:** Wengine pombe huwasababishia magonjwa mbalimbali.

Swali lilitoka katika mada ya Utungaji na lilimtaka mtahiniwa kupanga sentensi namba 40 kwa kuandika herufi moja wapo kati ya A, B, C na D katika mtiririko unaoleta mantiki ili kuunda kifungu cha habari chenye maana. Jedwali Na. 28 linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.

**Jedwali Na. 28: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo**

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 54,695 | 247,435 | 541,582 | 141,792 | 16,801 | 8,893 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 5.41 | 24.47 | 53.56 | 14.02 | 1.66 | 0.88 |

Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri kwa sababu watahiniwa 541,582 sawa na asilimia 53.56 walipanga sentensi hii katika mtiririko kwa kuipa herufi C ili kuunda habari fupi yenye mantiki. Watahiniwa hao walibaini kuwa sentensi hiyo ni ya tatu, kwa sababu sentensi ya 39 "watu waliotawaliwa na pombe hutumia pesa na muda mwingi kwenye pombe" ilikuwa inaelezea madhara ya pombe na sentensi ya 40 ni mwendelezo kuhusiana na madhara ya pombe kuwa huwasababishia magonjwa mbalimbali. Hivyo, watahiniwa hao walikuwa na maarifa na uelewa katika upangaji wa mawazo katika mtiririko wenye mantiki na kuunda kifungu cha habari.

Hata hivyo, watahiniwa 16,801 sawa na asilimia 1.66 walichagua herufi E isiyokuwa na sentensi yoyote kati ya sentensi zilizokuwa katika habari kutokana na kutokuelewa matakwa ya swali.

## 2.5 Sehemu E: Ufahamu

Sehemu hii ilikuwa na maswali matano yaliyohusu ufahamu ambapo mtahiniwa alitakiwa kutumia maarifa na weledi katika kusoma kwa makini na kuelewa kifungu cha habari kisha kujibu maswali kutokana na habari hiyo. Kifuatacho ni kifungu cha habari walichopewa watahiniwa.


> Wenyeji wa kijiji cha Gallu waliishi maisha ya kukosa maji na hali ya hewa ilikuwa ya joto sana. Hali hiyo haikuwepo zamani bali ilitokana na kuchoma nyasi na kukata miti bila kupanda mingine.

Waliposhauriwa na viongozi kupanda miti kumi ndipo wakate mmoja, walikaidi ushauri huo. Hali ilipozidi kuwa mbaya na ya kutisha, ilibidi viongozi wa kijiji pamoja na wazee wa hekima pale kijijini waitishe mkutano wa wakazi wote ili kujadili suala hilo.

Baada ya mazungumzo ya muda mrefu, walikubaliana kupanda miti robo tatu ya eneo lao na kuchimba lambo. Aidha walitunga sheria ndogondogo ili kudhibiti uharibifu wa mazingira. Miaka mitano ilipopita hali ya hewa ilibadilika na kuwa nzuri kama ilivyokuwa zamani. Kuanzia hapo uhifadhi wa mazingira ikawa ni desturi mojawapo katika jamii ile.

**Swali la 41:** Kichwa cha habari hii kingefaa kuwa kipi?


Swali hili lilitoka katika mada ya Ufahamu na lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika kusoma habari kwa ufahamu. Kielelezo Na 13 kinaonesha mtawanyiko wa alama za watahiniwa katika swali la 41.




Kielelezo Na 13*: Asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo*

Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani kwani watahiniwa 508,303 sawa na asilimia 50.40 walijibu kwa usahihi. Takwimu zinaonesha kuwa, watahiniwa hao walikuwa na maarifa

na ujuzi wa kutosha katika kusoma habari waliyopewa na hivyo kuandika kwa usahihi kichwa cha habari. Watahiniwa hao walionesha kuwa na wigo mpana wa majibu yao kutokana na kuelewa vyema kiini cha habari hiyo, hivyo waliandika kichwa cha habari kwa kutumia maneno yao yanayosadifu kichwa cha habari kwa usahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika kichwa cha habari "Utunzaji wa mazingira au umuhimu wa utunzaji wa mazingira". Kielelezo Na. 34 kinaonesha jibu zuri la mtahiniwa huyo aliyepata alama zote.


41. Kichwa cha habari hii kingefaa kuwa kipi?
Utunzaji wa Mazingira au umuhimu wa utunzaji wa mazingira.

*Kielelezo Na*. 14: *Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 41.*

Hata hivyo, watahiniwa 500,139 sawa na asilimia 49.6 walishindwa kubaini kichwa cha habari kutokana na kutokuelewa habari husika, hivyo kushindwa kubaini mawazo makuu yaliyomo kwenye habari kama vile: *Kijiji cha Gallu, mazingira, uhifadhi wa mazingira, umuhimu wa kutunza mazingira* na *kuhifadhi mazingira*. Watahiniwa hao waliandika taarifa zao za awali za karatasi ya kujibia mtihani kwenye swali husika na wengine waliandika jibu kinyume na taratibu za uandishi wa kichwa cha habari ambapo idadi ya maneno hayatakiwi kuzidi matano. Mtahiniwa huyo aliandika mistari mitatu yenye maneno kumi na tisa. Kielelezo Na 15 ni mfano wa jibu la mtahiniwa huyo.

41. Kichwa cha habari hii kingefaa kuwa kipi?

Ilibidi viongozi ~~Pamoja~~ wa kijiji pamoja wazee wa hekima pale kijijini waitishe mkutano wa wahari wote ili kujadili swara hilo

*Kielelezo Na.* 15: *Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 41*

Watahiniwa wengine walishindwa kuandika kichwa cha habari kinachofaa kutokana na kutokujua kusoma na kuandika, hivyo walijibu swali kwa kuandika maneno yasiyoeleweka. Kielelezo Na. 16 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeandika herufi zisizoeleweka badala ya kuandika kichwa cha habari kama vile, *uhifadhi wa mazingira, umuhimu wa kutunza mazingira na mazingira*.

41. Kichwa cha habari hii kingefaa kuwa kipi?

[illegible]


*Kielelezo Na.17*: *Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 41.*

**Swali la 42:** Wenyeji wa kijiji cha Gallu walikuwa na tatizo gani? Taja matatizo mawili.

(i) ____________________


(ii) ____________________

Swali hili lilitoka katika mada ya Ufahamu na lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika kusoma habari kwa ufahamu. Kielelezo Na 18 kinaonesha mtawanyiko wa alama za watahiniwa katika swali la 42.




Kielelezo Na 18*: Asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo*

Kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri kwani jumla ya watahiniwa waliopata alama 1 hadi 2 ni 895,699 sawa na asilimia 88.80. Watahiniwa hao waliweza kutaja matatizo ya wenyeji wa kijiji cha Gallu ambayo ni: *ukosefu wa maji/kukosa maji na hali ya hewa kuwa ya joto sana*. Hii inadhihirisha kuwa, watahiniwa walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya ufahamu na hivyo kusoma habari kwa umakini na kujibu maswali husika kwa usahihi. Kielelezo Na. 19 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kujibu swali kwa ufasaha kulingana na kifungu cha habari alichosoma.



42. Wenyeji wa kijiji cha Gallu walikuwa na tatizo gani? Taja matatizo mawili.


(i) Kukosa maji.

(ii) Hali ya hewa kuwa ya joto Sana.

*Kielelezo Na. 19: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 42.*

Hata hivyo uchambuzi unaonesha kuwa, watahiniwa 112,743 sawa na asilimia 11.20 walishindwa kutoa maelezo sahihi kwa kuwa hawakuweza kusoma habari kwa umakini na kutambua maudhui

yaliyomo. Baadhi yao walionesha kukosa stadi za kusoma na kuandika, na wengine kutokuelewa habari, hivyo kushindwa kuandika matatizo mawili ya wenyeji wa kijiji cha Gallu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika majibu sahihi ya swali namba 43 ambayo ni “kuchoma nyasi na kukata miti bila kupanda mingine” katika swali namba 42, hii inadhihirisha kuwa, mtahiniwa huyo hakuwa makini katika kujibu kwa kufuata matakwa ya swali. Kielelezo Na. 20 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali.


42. Wenyeji wa kijiji cha Gallu walikuwa na tatizo gani? Taja matatizo mawili.

(i) kuchoma nyasi

(ii) kukata miti bila kupanda Mingine


Kielelezo Na. 20: *Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 42*

**Swali la 43**. Ni mambo gani yalisababisha hali ya hewa kuwa ya joto sana katika kijiji cha Gallu? Taja mambo mawili.

(i) ____________________________________


(ii) ____________________________________

Swali hili lilitoka katika mada ya Ufahamu na lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika kusoma habari kwa umakini na kujibu maswali kwa usahihi. Kielelezo Na. 21 kinaonesha mtawanyiko wa alama za watahiniwa katika swali la 21.




Kielelezo Na 21*: Asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo*


Kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri kwani jumla ya watahiniwa waliopata alama 1 na hadi 2 ni 882,573 sawa na asilimia 87.50. Watahiniwa hao walitaja mambo mawili yaliyosababisha hali ya hewa kuwa ya joto sana katika kijiji cha Gallu kuwa ni, *kuchoma nyasi na kukata miti bila kupanda mingine.* Hii ilitokana na uwezo wao wa kusoma kwa umakini na kuelewa kifungu cha habari. Huu ni uthibitisho kwamba watahiniwa wengi walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu ufahamu, hivyo waliweza kubainisha mambo yaliyosababisha hali ya hewa kuwa ya joto sana katika kijiji cha Gallu. Kielelezo Na 22 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi kulingana na matakwa ya swali.


43. Ni mambo gani yalisababisha hali ya hewa kuwa ya joto sana katika kijiji cha Gallu? Taja mambo mawili.
(i) Kuchoma nyasi
(ii) Kukata miti bila kupanda mingine.

Kielelezo Na. 22: *Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 43*

Hata hivyo, watahiniwa 125,869 sawa na asilimia 12.50 walishindwa kutaja mambo mawili yaliyosababisha hali ya hewa kuwa ya joto sana katika kijiji cha Gallu hivyo kutoa majibu ambayo


hayahusiani kabisa na swali husika. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika aina za maneno kama vile, *vielezi* na *kiunganishi* badala ya kutaja mambo mawili yaliyosababisha hali ya hewa kuwa ya joto sana katika kijiji cha Gallu ambayo ni *kuchoma nyasi na kukata miti bila kupanda mingine*. Kwa ujumla, watahiniwa wa kundi hili walikosa maarifa ya ufahamu juu ya kilichoandikwa katika habari. Kielelezo Na 23 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kutoa majibu sahihi ya swali husika.


43. Ni mambo gani yalisababisha hali ya hewa kuwa ya joto sana katika kijiji cha Gallu? Taja mambo mawili.
(i) vielezi
(ii) kiunganishi

Kielelezo Na. 23: *Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 43.*


**Swali la 44:** Nini maana ya neno "lambo" kama lilivyotumika kwenye habari uliyoisoma?

Swali hili lilitoka katika mada ya Ufahamu na lililenga kupima uwezo wa watahiniwa katika kuelewa maana ya msamiati "lambo" kama ulivyotumika katika habari waliyoisoma. Kielelezo Na. 24 kinaonesha mtawanyiko wa alama za watahiniwa katika swali la 44.




Kielelezo Na 24*: Asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo*

Kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa hafifu kwani watahiniwa 804,549 sawa na asilimia 79.78 walishindwa kueleza maana sahihi ya neno "lambo" kama lilivyotumika katika habari waliyosoma. Baadhi yao walitoa matumizi ya "lambo" badala ya maana yake. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika lambo *ni sehemu ya kunyweshea mifugo*. Watahiniwa wengine waliandika ni *mfuko wa kuhifadhia kitu* wakihusianisha na mfuko wa plastiki aina ya "Rambo" ambao hauwezi kuoza kama taka zingine, na wengine waliandika kuwa lambo ni *shimo la kutupia takataka*. Kielelezo Na.25 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali.



44. Nini maana ya neno "lambo" kama lilivyotumika kwenye habari uliyoisoma?

Ni taka ambayo haiwezi kuoza kama taka nyingine

*Kielelezo Na. 25***:** *Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 44.*

Hata hivyo, watahiniwa 203,893 sawa na asilimia 20.22 waliweza kutoa maana ya neno "lambo" kama lilivyotumika katika kifungu cha

habari kuwa, *ni shimo lililochimbwa kwa ajili ya kuhifadhia maji*. Aidha, watahiniwa wengine walieleza kuwa ni eneo maalumu /sehemu inayotumika kutunzia maji ya mvua. Hivyo, watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kusoma kwa makini na kuelewa msamiati liotumika katika habari husika. Kielelezo Na. 25 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeweza kutoa maana ya neno “lambo” kwa usahihi.



44. Nini maana ya neno “lambo” kama lilivyotumika kwenye habari uliyoisoma?

Ni shimo lililochimbwa kwa ajili ya kuhifadhia maji

*Kielelezo Na*. *25*: *Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 44.*

**Swali la 45:** Mwandishi anasema “Hali ya hewa ilibadilika na kuwa nzuri.” Ni jambo gani muhimu lililosababisha mabadiliko hayo?

Swali hili lilitoka katika mada ya Ufahamu na lililenga kupima uwezo wa watahiniwa katika kusoma habari kwa umakini na kujibu maswali kwa usahihi. Kielelezo Na. 26 kinaonesha mtawanyiko wa alama za watahiniwa katika swali.




Kielelezo Na 26*: Asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo*


Kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri kwa kuwa watahiniwa 814,869 sawa na asilimia 80.80 waliweza kutoa majibu sahihi. Watahiniwa hao waliweza kutaja jambo muhimu lililosababisha hali ya hewa kubadilika na kuwa nzuri. Hivyo, walionesha kuwa na wigo mpana wa majibu kutokana na kuelewa vyema kiini cha habari hiyo. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kutaja mambo zaidi ya moja yaliyosababisha hali ya hewa kubadilika na kuwa nzuri kuwa, ni; *walikubaliana kupanda miti robo tatu ya eneo lao na kuchimba lambo. Aidha walitunga sheria ndogondogo ili kudhibiti uharibifu wa mazingira*. Kielelezo Na. 27 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali kwa usahihi.

45. Mwandishi anasema "Hali ya hewa ilibadilika na kuwa nzuri." Ni jambo gani muhimu lililosababisha mabadiliko hayo?

Walikubaliana kupanda miti robo tatu ya eneo lao na kuchimba lambo. Aidha walitunga sheria ndogondogo ili kudhibiti Uharibifu wa Mazingira.

*Kielelezo Na. 27: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 45.*

Hata hivyo, watahiniwa 193,573 sawa na asilimia 19.20 walishindwa kutaja jambo muhimu lililosababisha hali ya hewa kubadilika na kuwa nzuri kwa sababu walikosa maarifa ya kubaini maudhui katika kifungu cha habari walichosoma. Watahiniwa hao waliandika maneno yaliyokuwemo katika kifungu cha habari lakini hayana uhusiano na swali. Wengine walitoa tafsiri ya maneno "mabadiliko ya hali ya hewa". Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika: "kuchoma nyasi na kukata miti bila kupanda mingine" badala ya kutaja jambo lililosababisha hali ya hewa kubadilika na kuwa nzuri kama vile kuchimba lambo, kupanda miti, na kutunga sheria ndogondogo ili kudhibiti uharibifu. Kielelezo Na. 28 kinaonesha majibu yasiyo sahihi kutoka kwa mmoja wa watahiniwa.


45. Mwandishi anasema "Hali ya hewa ilibadilika na kuwa nzuri." Ni jambo gani muhimu lililosababisha mabadiliko hayo?

Kuchoma nyasi na kukata miti bilakupanda Mingine

*Kielelezo Na. 28*: *Jibu lisilo sahihi katika swali la 45.*

## 3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA UFAULU KWA WATAHINIWA KATIKA MADA MBALIMBALI

Mada zilizotahiniwa katika somo la Kiswahili ni *Sarufi*, *Lugha ya Kifasihi*, *Ushairi, Utungaji na Ufahamu*. Uchambuzi unaonesha kuwa, mada nne kati ya tano zilikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu. Mada iliyokuwa na kiwango cha juu zaidi ilikuwa ni *Ufahamu (65.54%), ikifuatiwa na* Ushairi (64.56%), *Lugha ya Kifasihi* (64.37%), *Sarufi* (62.38%) na ya mwisho katika kundi hili ilikuwa Utungaji (57.75%). Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, maswali matatu yaliyotahiniwa katika mada ya Ufahamu yalijibiwa vizuri zaidi, nayo ni swali la 42 (88.80%), 43 (87.50%) na 45 (80.80%). Katika mada ya *Sarufi*, swali la 11 lilijibiwa vizuri zaidi na kuwa na ufaulu wa alama (88.70%). Aidha, swali la 8, 10

na 19 yalijibiwa vizuri sana ambapo kiwango cha ufaulu kilikuwa zaidi ya asilimia 80, yaani (86.40%), (86.60%) na (82.60%) mtawalia. Pia, katika mada ya *Ushairi* maswali yaliyojibiwa vizuri zaidi ni swali la 32 (84.10%) na 35 (81.70%) wakati katika mada ya *Lugha ya Kifasihi* swali la 21 (82.90%) na 28 (83.80%) ndiyo maswali yaliyojibiwa vizuri zaidi. Aidha, maswali yote yaliyotoka katika mada ya Utungaji yalijibiwa kwa kiwango cha wastani.

Kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika mada kwa mwaka 2019 na 2020 kinaonesha kushuka katika mada nne kati ya tano zilizotahiniwa kwa mwaka 2020. Viwango vya ufaulu katika mwaka 2020 vikilinganishwa na mwaka 2019 vinaonesha kuwa; katika mada ya *Lugha ya Kifasihi* kiwango cha ufaulu kimepungua kutoka asilimia 78.37 hadi asilimia 64.37 hivyo ufaulu umeshuka kwa asilimia 14.00. Pia, katika mada ya *Ufahamu*, kiwango cha ufaulu kimepungua kutoka asilimia 71.74 hadi 65.54 ambapo ni pungufu kwa asilimia 6.20. Vilevile, katika mada ya *Sarufi* kumekuwa na kiwango pungufu cha ufaulu kwa asilimia 4.73 kutoka 67.11% hadi 62.38%. Aidha, ufaulu umepungua katika mada ya *Utungaji* kwa asilimia 3.60 kutoka 61.35% hadi 57.75%. Hata hivyo, kumekuwa na ongezeko la ufaulu kwa asilimia 0.53 kutoka 64.03% hadi 64.56% katika mada ya ushairi.

## 4.0 HITIMISHO

Uchambuzi wa mada unaonesha kuwa, kiwango cha ufaulu katika mada zote kwa mwaka 2020 ni kizuri japokuwa kumekuwa na kushuka kwa asilimia 5.60 ikilinganishwa na mwaka 2019 ambapo kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika mada zote kilikuwa asilimia 68.52 ikilinganisha na mwaka 2020 ambapo ni asilimia 62.92.

Vilevile, uchambuzi huu umebainisha changamoto zilizowafanya watahiniwa kushindwa kujibu baadhi ya maswali kwa usahihi. Miongoni

mwa changamoto hizo ni; kushindwa kutambua matakwa ya swali, kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu msamiati na aina za maneno. Dosari nyingine ni kuchagua jibu zaidi ya moja kinyume na maelekezo katika kujibu maswali mbalimbali. Pia kushindwa kupanga sentensi katika mtiririko unaoleta mantiki. Hii imesababishwa na watahiniwa kutokuwa na maarifa ya kutosha ya uandishi wa insha hususani katika kupanga mawazo kwa mtiririko unaoleta mantiki ili kuunda kifungu cha habari.

Ili kukabiliana na changamoto hizi, ni vyema juhudi za makusudi za ufundishaji na ujifunzaji zifanyike ili kuwawezesha wanafunzi kuwa na weledi na maarifa ya kutosha katika somo la Kiswahili ambalo pia ni lugha ya Taifa hapa nchini Tanzania.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuinua kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa katika Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi, mambo yafuatayo hayana budi kuzingatiwa:

(a) Walimu wanatakiwa kufundisha mada ya sarufi na kuweka msisitizo katika ufundishaji wa dhana ya msamiati katika Lugha ya Kiswahili, kubaini aina za maneno na kuunda sentensi zenye upatanisho wa kisarufi na matumizi ya lugha. Kwa kutumia mbinu ya kuwaweka wanafunzi katika vikundi kujadili aina za maneno, dhana ya msamiati na upatanisho wa kisarufi kwa kutumia njia ya bungua bongo, njia shirikishi na maigizo.

(b) Walimu wanatakiwa kuweka msisitizo katika ufundishaji wa mada ya utungaji wa habari na insha, hususani katika kupanga mawazo yenye mtiririko unaoleta mantiki. Kwa kutumia mbinu za ujifunzaji zifuatazo:

   (i) Wanafunzi wakae katika vikundi wajadili na wapange mawazo kimantiki ili wapate habari kamili.

(ii) Wanafunzi waelezee katika vikundi jinsi walivyopanga mawazo kimantiki na kupata habari kamili.

(c) Walimu wanatakiwa kuweka msisitizo katika ufundishaji wa mashairi kwa kuzingatia muundo wa utunzi wa shairi kwa kutumia mbinu ya kuwaweka wanafunzi katika vikundi. Hivyo, kutunga mashairi ya kimapokeo na kubainisha vina na mizani katika mashairi yao pamoja na kughani mashairi waliyoyatunga.

(d) Walimu wanatakiwa kutumia mbinu ya bungua bongo na maigizo kwenye ufundishaji wa matumizi ya lugha ya kifasihi katika methali, nahau, misemo na vitendawili, hususani katika kuelewa maana, miundo na matumizi yake katika Lugha ya Kiswahili.

(e) Walimu wanatakiwa kuwafundisha wanafunzi misingi madhubuti ya kusoma matini mbalimbali ili kuwajengea uwezo wa kufanya uchambuzi makini katika mada ya ufahamu. Kwa kutumia mbinu ya kuwaweka wanafunzi katika vikundi mbalimbali na kusomeana matini kwa sauti katika vikundi vyao.

**KIAMBATISHO A**

## ULINGANIFU WA UFAULU KWA WATAHINIWA KWA KILA MADA KATIKA PSLE 2019 NA PSLE 2020

| Na. | Mada | Mtihani wa 2020 | | | | Mtihani wa 2019 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Ufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa Ufaulu (%) | Maoni | Ufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa Ufaulu (%) | Maoni |
| | | Namba ya swali | (%) ya Ufaulu | | | Namba ya swali | (%) ya Ufaulu | | |
| 1. | Ufahamu | 41 | 50.40 | 65.54 | Vizuri | 41 | 78.28 | 71.74 | vizuri |
| | | 42 | 88.80 | | | 42 | 65.95 | | |
| | | 33 | 87.50 | | | 43 | 56.99 | | |
| | | 44 | 20.20 | | | 44 | 88.97 | | |
| | | 45 | 80.80 | | | 45 | 68.68 | | |
| 2. | Ushairi | 31 | 59.70 | 64.56 | Vizuri | 31 | 82.14 | 64.03 | vizuri |
| | | 32 | 84.10 | | | 32 | 77.49 | | |
| | | 33 | 59.80 | | | 33 | 60.40 | | |
| | | 34 | 72.80 | | | 34 | 84.52 | | |
| | | 35 | 81.70 | | | 35 | 47.81 | | |
| | | 36 | 29.30 | | | 36 | 31.91 | | |
| 3. | Lugha ya Kifasihi | 21 | 82.90 | 64.37 | Vizurii | 21 | 89.37 | 78.37 | Vizuri |
| | | 22 | 79.30 | | | 22 | 85.79 | | |
| | | 23 | 52.20 | | | 23 | 60.3 | | |
| | | 24 | 64.30 | | | 24 | 89.31 | | |
| | | 25 | 72.60 | | | 25 | 85.75 | | |
| | | 26 | 75.80 | | | 26 | 60.37 | | |
| | | 27 | 19.80 | | | 27 | 63.72 | | |
| | | 28 | 83.80 | | | 28 | 84.24 | | |
| | | 29 | 38.90 | | | 29 | 72.66 | | |
| | | 30 | 74.10 | | | 30 | 92.13 | | |
| 4. | Sarufi | 1 | 43.70 | 62.38 | Vizuri | 1 | 44.15 | 67.11 | vizuri |
| | | 2 | 63.20 | | | 2 | 52.65 | | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 3 | 66.40 | | | 3 | 30.30 | | |
| | | 4 | 28.60 | | | 4 | 75.61 | | |
| | | 5 | 59.60 | | | 5 | 88.71 | | |
| | | 6 | 41.20 | | | 6 | 82.50 | | |
| | | 7 | 68.00 | | | 7 | 35.59 | | |
| | | 8 | 86.40 | | | 8 | 45.45 | | |
| | | 9 | 60.20 | | | 9 | 59.02 | | |
| | | 10 | 86.60 | | | 10 | 81.10 | | |
| | | 11 | 88.70 | | | 11 | 82.49 | | |
| | | 12 | 46.70 | | | 12 | 73.27 | | |
| | | 13 | 74.20 | | | 13 | 84.20 | | |
| | | 14 | 28.70 | | | 14 | 78.90 | | |
| | | 15 | 55.10 | | | 15 | 77.01 | | |
| | | 16 | 80.40 | | | 16 | 79.09 | | |
| | | 17 | 55.60 | | | 17 | 72.78 | | |
| | | 18 | 62.40 | | | 18 | 78.79 | | |
| | | 19 | 82.60 | | | 19 | 49.75 | | |
| | | 20 | 69.50 | | | 20 | 70.75 | | |
| 5. | Utungaji | 37 | 64.80 | 57.75 | Wastani | 37 | 47.19 | 61.35 | vizuri |
| | | 38 | 67.10 | | | 38 | 53.06 | | |
| | | 39 | 45.50 | | | 39 | 82.18 | | |
| | | 40 | 53.60 | | | 40 | 63.03 | | |

## KIAMBATISHO B

